# Nipashe

Jumatano Novemba 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581481

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital | epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




UKURASA 22

**UNITED WAHOFIA KUKOSA NNE BORA**



# Mafanikio makubwa

• **Muhimbili** yafanya upasuaji kupunguza matumbo makubwa, watumia dakika 30 hadi 90... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 3

**MAOFISA POLISI MBARONI MADAI YA UNYANG'ANYI, WIZI WA MILIONI 90/-**

MAOFISA watatu wa Jeshi la Polisi wamefikishwa katika Mahakama...

UKURASA WA 4

**TMA YASISITIZA UWAPO WA EL - NINO, YATOA TAHADHARI**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesisitiza uwapo wa mvua...

## Ujerumani yaipongeza Tanzania kwa utawala bora

UKURASA 3



Madaktari bingwa wabobezi wa upasuaji, wakiwamo wa mfumo wa chakula, ini na wataalamu wa operesheni za matundu wakifanya upasuaji wa mmoja wa watu waliopatiwa huduma ya kupunguza uzito katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dar es Salaam jana. **PICHA: MNH**



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mgeni wake, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier wakiangalia burudani ya ngoma za utamaduni, baada ya kuwasili Ikulu, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**


## Mwinyi aanika Z'bar ilivyopaa kwa miaka mitatu, aahidi neema zaidi

UK. 2



**MICHEZO** BALOZI UINGEREZA AONGEZA MZUKA DABI UK.24

**KATUNI** UK.6




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhi cheti kwa Meneja wa Biashara wa Benki ya NMB Zanzibar, Naima Said Shaame, cha kutambua mchango wa benki hiyo, wakati wa kongamano la kujadili miaka mitatu ya mafanikio, fursa na changamoto tangu aingie madarakani jijini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafanikio MNH upasuaji wa kupunguza matumbo

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, imewafanyia upasuaji wanawake wanne kwa kupunguza tumbo, kudhibiti uzito uliokithiri kati ya kilo 107 na 142.

Upasuaji huo ambao ulichukua kati ya dakika 30 hadi saa moja na nusu kila mmoja, ulifanywa na madaktari bingwa wabobezi wa upasuaji wa hospitali hiyo kwa kushirikiana na mabingwa kutoka India, Dk. Mohit Bhandari na Taasisi ya Medincredi.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, aliyesema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu upasuaji huo wa kwanza nchini, huku akibainisha kuwa watu hao walikuwa na uzito uliokithiri hatua ya tatu.



"Umri wao ni kati ya miaka 36 na 40 tuliowafanyia upasuaji. Kwa umri huo utaona bado ni vijana. Uzito si ugonjwa ila ni dalili ya ugonjwa na ukiona una uzito mkubwa wa kupitiliza kama huu ni kwamba una kitu kinasababisha.

Prof. Janabi alisema uzito kwa waliopatiwa huduma hiyo, utaanza kupungua taratibu kati ya asilimia 20 na 30 kwa kipindi cha miezi 12 hadi 24, akisisitiza kuhudhuria kliniki, kuacha kula vitu vyenye sukari, kufanya mazoezi, kupunguza vyakula vya wanga na kuzingatia muda wa kupumzika.

"Pia uzito huo unaweza kuwa na athari, ugonjwa wa kisukari na kushindwa kupata mtoto. Sasa hivi ugumba umekuwa shida na kinababa wanapata tatizo la uume kutofanya kazi, magonjwa ya moyo na kiharusi," alisema.

Prof. Janabi alisema upasuaji huo wa kibingwa uliofanyika kwa njia ya matundu madogo na endoskopia, ni utekelezaji wa jukumu la hospitali hiyo katika matibabu bobezi na kuhakikisha huduma nyingi zinafanyika nchini. Alisema upasuaji huo unagharimu takribani Sh. milioni 15 kwa mtu mmoja.

"Kuna njia nne za upasuaji huu ila tuliyoitumia ni kati ya hizo. Wagonjwa hawa baada ya upasuaji, mmoja aliruhusiwa na wengine waliruhusiwa siku iliyofuata. Takwimu za dunia zinaonyesha watu 380,000 wamefanyiwa upasuaji kama huu.

"Kwa Tanzania kufanya upasuaji huu, tumeingia katika historia. Ukiwa na uzito mkubwa unahatarisha maisha. Ukiwa na kisukari, tatizo ni chakula, ukidhibiti chakula ndipo vitafuata vidonge, sindano. Nje ya nchi, upasuaji huu ni kati ya dola 22,000 ukizidisha unapata Sh. Mil. 50 hadi 70," aliongeza Prof. Janabi.

Alisema upasuaji wa aina hiyo, utafanyika kwa mara nyingine mwezi huu kwa kushirikiana na bingwa huyo kutoka India, ili kuwaongezea uzoefu mabingwa wa ndani ambao watatoa huduma hiyo wenyewe hapo baadaye.

"Upasuaji huu hatari yake ni ndogo kuliko kufanyiwa upasuaji kwani ukiwa na uzito mkubwa utapata mshtuko wa moyo, figo zitaharibika, utatakiwa kusafishwa figo gharama ni kubwa.

"Ninachosisitiza ni kuacha kula mara kwa mara. Ukila asubuhi subiri hadi mchana saa 6:00 na baada ya hapo kula saa 1:00 hadi saa 2:00 usiku. Usile kwa sababu muda wa kula umefika, kula ukiwa na njaa," alisema.

Kuhusu huduma ya kuwekewa puto iliyoanzishwa hospitalini hapo Desemba, mwaka jana, Bingwa wa Upasuaji wa Hospitali hiyo, Dk. Eric Muhumba, alisema watu 150 wamepatiwa huduma hiyo kwenye tumbo la chakula ili kudhibiti uzito uliokithiri.

# Rais Mwinyi aanika mafanikio miaka mitatu, aahidi makubwa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameanika mafanikio katika muda wa miaka mitatu tangu aingie madarakani huku akiahidi kuendelea kuzuia na kudhibiti uvujaji mapato ili kuboresha maendeleo kwa maslahi mapana ya nchi.

Amesema katika miaka hiyo mitatu, maendeleo makubwa yaliyopatikana, yametokana na kuimarika kwa mifumo ya kidijitali inayodhibiti matumizi na fedha za serikali kupotea katika maeneo yote yakiwamo viwanja vya ndege, bandarini na halmashauri.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana visiwani hapa kwenye kongamano la maadhimisho ya miaka mitatu ya uongozi wake.

Alisema ndani ya kipindi cha miaka mitatu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa utawala bora wenye kufuata katiba ya nchi, sheria, kanuni, kuwashirikisha watu na kufanya uamuzi sahihi kwa maslahi mapana ya nchi na watu wake.

Rais Mwinyi alisema hali hiyo imeimarisha amani, utulivu na mshikamano wa Wazanzibari bila kujali tofauti zao za kisiasa, dini na maeneo wanayotoka katika kujenga maendeleo ya pamoja.

Dk. Mwinyi alisema hali ya utulivu wa nchi iliyopo sasa, imewavutia wawekezaji wengi waliowekeza mitaji mikubwa kwenye sekta za utalii na uwekezaji.

"Wawekezaji wanajali zaidi amani ya nchi wanayotaka kuwekeza mitaji yao. Sisi bahati nzuri nchi yetu inafuata taratibu, sera na sheria za kumlinda mwekezaji," alisema.

Kuhusu mafaniko ya utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu, Dk. Mwinyi alisema yametokana na sekta tano ambazo ni utalii, uvuvi na ufugaji, bandari, mafuta na gesi pamoja na biashara kupitia usafiri wa majini.

Alisema mafanikio makubwa yamepatikana na Zanzibar inaongoza kupokea ndege kubwa za kimataifa zinazoingiza watalii wengi kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Pia alisema serikali inatekeleza miradi mikubwa pia wawekezaji wengi wanainufaisha Zanzibar kwa kuongeza soko la ajira kwa wazawa kupitia utalii, uvuvi, ufugaji, kilimo cha mwani, bandari na biashara za majini baina ya bandari za Unguja na Pemba, Dar es Salaam, Tanga, Kilwa, Mombasa na Comoro, kwa kukuza biashara kubwa na ndogo, kukua kwa soko la bidhaa zinazozalishwa nchini na kuongezeka kwa makusanyo ya kodi yenye tija kwa maslahi mapana ya nchi.

Alisema serikali imewekeza mitaji mikubwa kwa ajili ya wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo yenye thamani ya Sh. bilioni 31 na zaidi ya dola za Marekani milioni 10 (sawa na shilingi bilioni 25) kutoka kwa Mfuko wa Khalifa pamoja na kuboresha mazingira mazuri kwa wafanyabiashara kutokana na ujenzi wa masoko ya kisasa ya Mwanakwerekwe, Mombasa, Jumbi na Chuini na maeneo mengine ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi pia alieleza serikali ilivyochukua hatua dhidi ya kero za badari ya Malindi na mfumko wa bei za bidhaa kwa kuruhusu kuruhusu sekta binafsi kuedesha bandari hiyo sambamba na serikali kuendelea na ujezi wa bandari jumuishi ya Mangapwani, Kaskazini Unguja itakayokidhi haja kwa matumizi ya bandari za kisasa.

Kwa miaka miwili ijayo ya ngwe yake ya kwanza ya uongozi wake, Rais Dk. Mwinyi aliahidi kuongeza kasi zaidi ya maendeleo ili kukamilisha ahadi alizoziweka kwa Zanzibar.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema Wazanzibari wanashuhudia maendeleo makubwa yaliyofikiwa katika kipindi kifupi cha miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Mwinyi.

Alisema, Dk. Mwinyi ametekeleza ahadi zake kwa vitendo kama alivyoahidi wananchi wakati anaingia madarakani.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, alisifu juhudi kubwa za maendeleo zilizofanywa ndani ya miaka mitatu kuwa ni za kupigiwa mfano hasa kwenye kuimarika kwa huduma za jamii hususani afya, elimu, makazi na maji safi na salama.

# Ujerumani yaipongeza Tanzania kwa utawala bora

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier, ameahidi nchi yake kuendelea kushirikiana na Tanzania kwenye sekta mbalimbali huku akipongeza jitihada zilizofanywa kwenye ujenzi wa uchumi, utawala wa sheria na demokrasia.

Amesema ziara yake nchini, atawatembelea wahanga wa Vita ya Majimaji pamoja na kuangalia namna ya kuwa na simulizi mpya baada ya ukoloni.

Rais Steinmeier aliyasema hayo jana Ikulu, jijini Dar es Salaam, baada ya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari, Steinmeier alisema ujio huo umepokewa vizuri na Ujerumani kwa kuwa, wameona namna (Rais Samia) alivyoweza kujenga uchumi, utawala wa sheria na kazi kubwa iliyofanyika eneo la demokrasia.

"Tunapenda kuwahakikishia sisi watu wa Ujerumani tunakwenda kusimama na nyinyi na tutaendelea kuwa washirika wa pamoja na kwa ukaribu, urafiki ambao umekuwapo kwa miaka kadhaa utaendelea kwa sababu ya uaminifu uliopo kati ya nchi hizo.

Aliahidi kuendelea kuwekeza katika ukanda huo na kusema alivyofurahishwa na Rais Samia katika kudumisha uhusiano na kufanya uwe mzuri zaidi kwa ajili ya kesho.

"Tumejadiliana namna gani uhusiano huu unaweza kuwa na nguvu zaidi kuweza kuvuka mipaka ya kisiasa. Namna gani tunaweza kuendelea kujenga uhusiano zaidi katika maeneo mengine ya ushirikiano, Rais alitaja pia, suala la rasilimali, kilimo, afya na nishati mbadala ambayo ni sekta muhimu sana.

"Kule Ujerumani tuko katika mchakato mzito sasa wa kubadilisha mfumo wa kuangalia namna gani kutokana na mabadiliko ya tabianchi, tupunguze matumizi makubwa ya hewa ukaa katika suala zima la nishati na maarifa ya nishati mbadala. "Tutaona namna gani ya kushirikishana maarifa katika sekta hii kwa maana tunajua mtu yeyote ambaye anataka kutumia nishati mbadala lazima awe na maarifa ya kuitumia," alisema.

Vilevile, alisema wana matumaini ziara hiyo italeta matunda katika uhusiano na kiuchumi na sekta mbalimbali.

Katika safari zake mbili Tanzania, alijifunza kuwa kuna kampuni nyingi changa za uwekezaji na anatazamia kukutana na wabunifu kuona namna ya kutoa mitaji zaidi na kuwasaidia katika eneo la uzoefu ili kuwa na wabobezi wa uchumi wa kidijitali na kutengeneza ajira kwa kizazi kijacho.

"Tumejadiliana namna gani ushirikiano ulipo tuuendeleze na bila kusahau uliopita. Tuna ushirikiano wa karibu, lakini pia tuna jana iliyofanana kutokana na mambo tuliyopitia wakati wa ukoloni.

"Ni muhimu tuweze kukubaliana na kufikia uamuzi wa kufanya utafiti wa ndani na kuongeza maarifa katika hiki kitu kilichotokea katika ukoloni na kuona namna ya kuangalia yaliyopita na kuangalia ukurasa mpya," alisema.

**VITA MAJIMAJI**

Alisema katika ziara hiyo ataangalia yaliyotokea na kuwaona walioathiriwa na vita ya Majimaji na kukutana na kuongea na baadhi yao kwa kuwa, anajua walipitia kipindi kigumu ambacho si cha kupendeza.

"Nitakwenda kuwaona na yote watakayonieleza nitakwenda kuyarudisha Ujerumani. Tuangalie namna ya kurudisha yale mabaki yaliyopo kule (Ujerumani)," alisema.

Rais Samia alimshukuru mgeni wake kwa kukubali mwaliko wake wa kutembelea Tanzania ambayo ameitaja kuwa ni ishara njema ya umuhimu wa uhusiano kati ya nchi hizo.

Rais Samia alisema wamepata fursa ya kuzungumza mambo mbalimbali akiyataja baadhi kuwa ni ushirikiano wa kijamii na kiuchumi na uhusiano kati ya nchi hizo uliofikia miaka 60.

"Katika mazungumzo yetu leo (jana), tumezielekeza timu za wataalam wa Tanzania na Ujerumani kuendelea na mzungumzo pamoja na mashauriano ya mara kwa mara yanayolenga kuboresha maeneo yaliyopo ya ushirikiano na kuibua maeneo mengine mapya yenye umuhimu kwa uchumi wa nchi zetu mbili," alisema.

Pia, alimhakikishia kuwa Serikali ya Tanzania ipo tayari kuwa mwenyeji wa mazungumzo yajayo ya ushirikiano wa maendeleo yatakayofanyika mwakani (2024).

Upande wa biashara na uwekezaji, alisema wamesisitiza umuhimu wa biashara na uwekezaji katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

"Tumekuwa na miradi si chini ya 178 au 180 ya Ujerumani katika ngazi mbalimbali iliyowekezwa Tanzania. Tunafanya biashara na Ujerumani, kuna uwezekano mkubwa wa kukuza biashara na hilo ndilo tutalielekeza katika mazungumzo yajayo," alisema.

Rais Samia aligusia pia, kongamano la wafanyabiashara wa Tanzania na Ujerumani ambalo lilifanyika jana jijini Dar es Salaam huku akieleza kuwa, fursa zote za uwekezaji na biashara zimezungumzwa na watakaokubaliana wataingia katika mikataba ya makubaliano.

Alisema katika sekta ya utalii, upo uwezekani wa kupata watalii wengi zaidi kutoka Ujerumani watakapojitangaza vizuri kwao.

Kuhusu uhifadhi, Alisema Frankfurt Zoological Society na mashirika mengine ya Ujerumani yamekuwa yakisaidia kwenye eneo hilo katika mbuga hasa Selous na Serengeti na kuna Mradi wa Serengeti Ecosystem wanaofanya kazi pamoja.

Kadhalika, wamezungumzia mambo ya kihistoria na wapo tayari kufungua majadiliano na kuona watakavyoweza kukubaliana kwa yale yaliyopita wakati wa utawala huo.

"Tunajua kuna familia ambazo zinasubiri mabaki ya wapendwa wao ambao wapo kule katika makumbusho mbalimbali za Ujerumani. Yote haya tunakwenda kuyazungumza na kuona vipi twende nayo vizuri.

"Nimezungumza naye pia, Tanzania tunaangalia usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, tumezungumza kupitia mradi tunaoutekeleza kama itawezekana tushirikiane," alisema.

Maeneo mengine aliyoyataja ni masuala ya demokrasia na haki za binadamu, utawala wa sheria na utawala bora ambao Rais wa Ujerumani, ameipongeza Tanzania kuwa imeonekana kutulia kwenye utawala wa sheria na utawala bora.

"Ndiyo maana wamevutika wafanyabiashara wa Ujerumani kuja Tanzania kuangalia fursa za uwekezaji. Kubwa lingine yanayokuja sasa ni kujenga uwezo wa vijana kwenye uchumi wa kidijitali.

Rais Samia alisema ziara hiyo inathibitisha dhamira ya dhati ya serikali hizo kuimarisha na kukuza ushirikiano na urafiki kwa lengo la kunufaisha watu.

Alisema Ujerumani inashirikana na Tanzania katika sekta mbalimbali na inajenga hospitali kubwa ya jeshi jijini Dodoma na nyingine ya kisasa ya maradhi ya kuambukiza, Lugalo jijini Dar es Salaam.

## Maofisa polisi mbaroni madai ya unyang'anyi wizi mil. 90/-

**Na Kulwa Mzee**

MAOFISA watatu wa Jeshi la Polisi wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za unyang'anyi wa kutumia silaha na kuiba Sh. milioni 90.

Washtakiwa hao ni Koplo Ramadhani (42) maarufu Rasta, Koplo Majid Abdallah (35) na Koplo Stella Mashaka (40).

Wakili wa Serikali, Neema Moshi, aliwasomea washtakiwa hao shtaka moja la unyang'anyi linalowakabili, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Amir Msumi.

Alidai washtakiwa kwa pamoja Agosti 28, mwaka huu, maeneo ya Kurasini, jirani na Ofisi ya Uhamiaji, wilayani Temeke, waliiba Sh. milioni 90.

Wakili Neema alidai washtakiwa kabla na baada ya kuiba fedha hizo, walimtishia kwa bunduki Grace Matage kwa nia ya kujipatia fedha hizo.

Baada ya kusomewa mashtaka washtakiwa wote walikana kutenda makosa hayo, upande wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika na kuomba kesi iahirishwe hadi tarehe nyingine.

Upande wa washtakiwa haukuwa na pingamizi, mahakama iliahirisha shauri hilo hadi Novemba 13, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Msumi aliamuru washtakiwa warudishwe rumande hadi tarehe hiyo kwa sababu shtaka linalowakabili halina dhamana.

Kamal

KAMAL GASES LIMITED

TAARIFA KWA UMMA

Sisi **Kamal Gases limited** wazalishaji namba moja wa gesi za viwandani zenye ubora uliothibitika na Shirika la viwango Tanzania TBS.

Tumegundua kuwepo kwa wazalishaji wa gesi wanaotumia mitungi yenye nembo ya KGL kinyume na sheria.

Tunawatangazia wazalishaji, watumiaji wa gesi za viwandani na umma kwa ujumla kwamba ni kinyume cha sheria kujaza, kuuza, na kusambaza gesi iliyowekwa kwenye mitungu yenye nembo ya kamal ambayo haikuzalishwa na Kamal Gases Limited.

Hivyo mnahabarishwa kwamba; Kamal Gases Limited wapo katika zoezi kabambe la kufuatilia na kukamata wahusika wote wanaozalisha gesi za viwandani na kujaza katika mitungi yenye nembo au alama ya kamal gases limited kinyume cha utaratibu.

Kamal Gases Limited itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufungua kesi za madai na jinai kwa yoyote atakaye tumia mitungi ya gesi yenye nembo ya Kamal Gases Limited kujaza gesi aliyoichakata mwenyewe au iliyochakatwa na wazalishaji wengine nje ya Kamal Gases Limited

Tunatoa wito kwa wateja wetu kuendelea kutumia huduma ya gesi ya Kamal Gases Limited kwa kupitia vituo vilivyoidhinishwa na kuitambulika na Kamal Gases Limited au wafike kiwandani chang'ombe industrial area plot no. 188/2 kwa maelezo zaidi piga simu namba **+255 765 169 444**

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kamal Gases Limited**
**Dar es Salaam**

# Mke wa Bilionea Msuya adai hakuwa na mali alipoolewa

Na Grace Gurisha

ALIYEKUWA mke wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha maarufu Bilionea Msuya, Miriam Mrita, ameieleza mahakama kabla ya kuolewa hakuwa na mali na anafahamu baba mkwe wake alikuwa na machimbo ya Tanzanite.

Aidha, amedai anafahamu mgodi wa Tanzanite ni wa kwake na hafahamu jina la mgodi ambao marehemu mume wake Erasto na baba mkwe wake Elisaria waliokuwa wakichimba pamoja.

Alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati akijibu maswali ya dodoso kutoka kwa Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, baada ya kumaliza kutoa utetezi wake wa tuhuma za kifo cha wifi yake, Aneth Msuya.

Akimuuliza maswali hayo, Kimweri alimtaka Mrita amjibu maswali kama anavyomuuliza, kwa sababu alitoa ushahidi wake mrefu akipinga tuhuma zinazomkabili.

**Kimweri:** Tuanze kwa kukumbusha majina yako.

**Mrita:** Miriam Steven Mrita.

**Kimweri:** Kiwango chako cha elimu cha juu.

**Mrita:** Ni darasa la saba

**Kimweri:** Uliolewa lini na marehemu Erasto Msuya

**Mrita:** 1996

**Kimweri:** Wakati unaolewa ulikuwa hauna ajira rasmi, yaani kwa kiswahili rahisi uliolewa kama mama wa nyumbani.

**Mrita:** Sijaelewa swali.

**Kimweri:** Swali langu ni jepesi sana ulikuwa na ajira rasmi?

**Mrita:** Sijaelewa swali.

**Kimweri:** Mheshimiwa Jaji naomba ajibu swali kama alikuwa na ajira rasmi?

**Kimweri:** Haya narudia tena mbona swali rahisi tu ulikuwa na ajira rasmi?

**Mrita:** Sijaelewa.

**Kimweri:** Nakuuliza kwa mara ya mwisho, ambapo nitataka mwongozo wa jaji katika hili, haya wakati unaolewa ulikuwa na ajira rasmi?

**Mrita:** Nilikuwa sina ajira rasmi.

**Kimweri:** Kwenye ushahidi wako ulioutoa hapa mahakamani mrefu sana, ulitaja biashara nyingi zikiwamo machimbo ya madini, sasa swali, hizi biashara ulizozitaja kabla ya kuolewa na Erasto ulikuwa nazo?

**Mrita:** Sijaelewa.

**Kimweri:** Narudia tena kabla ya wewe kuolewa na Erasto mali hizo ulizozitaja ulikuwa nazo?

**Mrita:** Baada ya kuolewa.

**Kimweri:** Sijakuuliza baada, nimekuuliza kabla hujaolewa hizo mali ulikuwa nazo?

**Mrita:** Sijaelewa swali hebu rudia.

**Jaji:** Shahidi swali ni rahisi tu, kabla hujaolewa ulikuwa na hizo biashara?

**Mrita:** Ilikuwa bado.

**Kimweri:** Hizi biashara umehusika nazo baada ya kuolewa.

**Mrita:** Sio kweli Mheshimiwa Jaji.

**Kimweri:** Baada ya kuolewa na familia ya Elisaria Elia Msuya uliwahi kufahamu kwamba baba mkwe wako alikuwa akimiliki migodi ya Tanzanite?

**Mrita:** Mgodi wa Tanzanite ninachofahamu ni wangu.

**Kimweri:** Swali langu ni kwamba ulikuwa unajua kama baba mkwe wako anamiliki mgodi?

**Mrita:** Alikuwa mchimbaji wa Tanzanite.

**Kimweri:** Mbona swali langu ni jepesi sana shahidi, ulikuwa unajua kama anamiliki?

**Mrita:** Ndiyo na pia alikuwa mchimbaji, walikuwa wanachimba yeye na mtoto wake (Erasto).

**Kimweri:** Uliweza kujua kama mgodi huo ulikuwa ni wa Elisaria?

**Mrita:** Kama ulikuwa wa kwake au sio, mi sijui.

**Kimweri:** Huu mgodi unaitwaje, kwa sababu ulitaja migodi hapa.

**Mrita:** Mgodi ulikuwa mmoja umesajiliwa kwa jina la Erasto na mwingine Elisaria.

**Kimweri:** Unafahamu umesajiliwa kwa jina gani kwa sababu umesema mgodi ni mmoja.

**Mrita:** Huo mgodi wa baba na mtoto wake sijui umesajiliwa kwa jina gani.

**Kimweri:** Ulipokuwa na Erasto mlikuwa mnamiliki magari kadhaa.

**Mrita:** Kweli.

Kimweri: Unaweza kukumbuka haya magari yalikuwa ni ya aina gani.

**Mrita:** Erasto alikuwa na gari lake na mimi la kwangu.

**Kimweri:** Ngoja nikukumbushe kupitia kielelezo chenu kutoka TRA, gari namba T 429 BYY aina ya Range Rover ilikuwa ni miongoni mwa magari mliyokuwa mkimiliki.

**Mrita:** Mheshimiwa Jaji ningeoneshwa kwanza ndiyo nijibu.

**Kimweri:** Mbona swali rahisi sana tu nimekuuliza hilo gari ni miongoni mwa magari ambayo mlikuwa mnayamiliki.

**Mrita:** Sikumbuki kama tulikuwa tunamiliki gari kama hilo.

**Kimweri:** Khe! Hukumbuki haya sawa ngoja liingie kwenye kumbukumbu.

**Mrita:** Samahani Mheshimiwa Jaji nakumbuka mume wangu alikuwa na gari aina ya Range Rover Evoque, lakini sikumbuki namba zake.

**Kimweri:** Ngoja nikukumbushe gari namba T 677 BNM Land Cruiser, haya vipi kuhusu hili na lenyewe lilikuwa ni miongoni mwa gari mnazomiliki?

**Mrita:** Baada ya...

**Kimweri:** Baada ya nini shahidi?

**Mrita:** Sikumbuki.

**Kimweri:** Vipi kuhusu hili T 307 CBH Ford Range

**Mrita:** Nakumbuka gari hili lilisajiliwa kwa jina langu.

**Kimweri:** Ooh! Hili umelikumbuka eeh.



**Mrita:** Ndiyo.

**Kimweri:** Vipi kuhusu gari namba T 800 CKF aina ya Range Rover.

**Mrita:** Sikumbuki.

**Kimweri:** Kwa hiyo wewe hujawahi kumilikii gari kama hili.

**Mrita:** Kimya

**Kimweri:** Unakumbuka siku Erasto anapigwa risasi na kufariki, alikuwa akiendesha gari hilo.

**Mrita:** Sikumbuki.

**Kimweri:** Lakini unakumbuka tukio la mwili ulipokutwa pembeni ya gari alilokuwa akiliendesha?

**Mrita:** Nakumbuka mume wangu alipigwa risasi na kuawa.

**Kimweri:** Swali langu ni simple unakumbuka hilo tukio?

**Mrita:** Wakati tunapata taarifa mwili tayari ulikuwa mochwari.

**Kimweri:** Swali langu unakumbuka.

**Mrita:** Sikumbuki.

**Kimweri:** Kwahiyo kwa ujumla wakati anafariki alikuwa na magari mangapi?

**Mrita:** Sikumbuki.

**Kimweri:** Kwenye hichi kielelezo cha uchunguzi wa magari kutoka TRA, hebu soma mmiliki wa mwisho wa gari hilo ni nani namba T 800 CKF.

**Mrita:** Miriam Steven Mrita.

**Kimweri:** Baada ya kusoma umekumbuka eeh.

**Mrita:** Ndiyo nimekumbuka.

**Kimweri:** Tarehe 12/12/2013 kwa mujibu wa taarifa ndiyo mara yako ya kwanza wewe kuanza kumiliki gari hilo.

**Mrita:** Ndiyo.

**Kimweri:** Hii ilikuwa ni muda gani baada ya mume wako kufariki.

**Mrita:** Miezi mitano.

**Kimweri:** Unakumbuka hii gari namba T 800 CKF marehemu Erasto aliiendesha mara ya mwisho.

**Mrita:** Sikumbuki.

**Kimweri:** Wakati unafanya mabadiliko ya mmiliki wa gari hilo, ulishateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi.

**Mrita:** Ndiyo nilikuwa nimeshateuliwa.

**Kimweri:** Ni lini ulianza kuwa msimamizi wa mali.

**Mrita:** 5/11/2013.

**Kimweri:** Na wakati unateuliwa mahakama ilikupa maelekezo kwamba ndani ya miezi sita uwe umepeleka mrejesho wa mali?

**Mrita:** Ndiyo nakumbuka ilielekeza hivyo.

**Kimweri:** Ndani ya miezi sita?

**Mrita:** Ndiyo miezi sita.

**Kimweri:** Kuanzia tarehe 5/11/2013 ulipochaguliwa kuwa msimamizi wa mali hadi Agosti 5, 2016 ulikuwa bado hujapeleka orodha hiyo mahakamani?

**Mrita:** Nilishalijibu hilo swali.

**Kimweri:** Jibu swali.

**Mrita:** Ndiyo (alijibu kwa sauti ya chini).

**Kimweri:** Mheshimiwa Jaji sijui kama jibu limeeleweka.

**Jaji:** Hadi anakamatwa alikuwa bado hajapeleka.

**Kimweri:** Wakati unafanya mabadiliko ya umiliki wa gari namba T800 CKF ulikuwa bado hujapeleka mrejesho.

**Mrita:** Sikumbuki.

**Kimweri:** Hukumbuki nini?

**Mrita:** Usitake nijibu unachotaka wewe.

**Kimweri:** Tarehe 12/12/2013 ambayo ndiyo ulianza kumiliki hilo gari, ulikuwa umeshafaili mrejesho mahakamani.

**Mrita:** Bado.

Kesi inaendelea leo kwa Mrita kuulizwa maswali ya dodoso na upande wa mashtaka.

# TMA yasisitiza uwapo wa El-Nino

Na Faustine Feliciane

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesisitiza uwapo wa mvua za El-Nino na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza.

Aidha, TMA imetoa utabiri wa mvua za wastani mpaka juu ya wastani kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka. Mikoa hiyo ni Kigoma, Rukwa, Katavi, Tabora, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma na eneo la kusini mwa Morogoro.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chan'ga, alisema jana kuwa kipindi cha nusu ya msimu (Novemba, mwaka huu hadi Januari, mwakani), kinatarajiwa kuwa na mvua nyingi kulinganisha na nusu ya pili (Februari hadi Aprili, 2024) na kwamba uwapo wa El-Nino unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika mvua za msimu.

Dk. Chang'a alibainisha athari zinazoweza kujitokeza kuwa ni vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi na mafuriko yanayoweza kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo. Pia alisema kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kuongezeka kutokana na mvua hizo.

Alisema katika mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka, mvua zilitarajiwa kuanza kunyesha wiki ya mwisho ya Oktoba na wiki ya kwanza ya Novemba na zinatarajiwa kumalizika wiki ya nne ya Aprili, 2024.

Dk. Chang'a pia alisema msimu wa vuli kwa miezi ya Oktoba hadi Desemba, mwaka huu, katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa Morogoro, Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia) na Zanzibar (visiwa vya Unguja na Pemba) utabiri wake ulitolewa Agosti 24, mwaka huu.

Alisema mvua hizo zimeshaanza katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, pwani ya kaskazini na baadhi ya maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki kama ilivyotabiriwa.

Pia alisema ongezeko la mvua linatarajiwa Novemba na Disemba, mwaka huu na mvua za nje ya msimu zinatarajiwa kuwapo Januari na Februari, 2024.

"Watu wandelee kuchukua tahadhari kama tunavyosisitiza, mifumo ya hali ya hewa pia bado inaonyesha uwapo wa El Nino. Wananchi na mamlaka husika ziendelee kuchukua tahadhari," alisema Dk Chang'a huku akibainisha kuwa miongoni mwa athari zinazotarajiwa ni mafuriko katika mikoa mingi, hivyo tahadhari zichukuliwe kukabiliana na hali hiyo.

Mara ya mwisho mvua za El Nino zilinyesha msimu wa mwaka 2018/19 ambazo zilikuwa El Nino dhaifu kulinganisha na El Nino ya mwaka 1997-1998.

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuimarishwa usalama viwanja vya ndege kipaumbele muhimu

**MAMLAKA** ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) juzi iliadhimisha miaka 20 tangu ilipoanzishwa huku ikibainishwa kuwa kumekuwa na mafanikio makubwa ya kiutendaji ikiwamo udhibiti wa usafiri katika viwanja vya ndege. Hatua hiyo imesababisha kuwa katika moja ya mamlaka bora kwa udhibiti katika usafiri wa anga kikanda na kimataifa.

Hayo ni mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yaliyowekwa kwa mujibu wa iliyounda mamlaka hiyo, pamoja sheria zinazoongoza tasnia kama zilivyoainishwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO).

Pamoja na mafanikio hayo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyekuwa mgeni rasmi, aliitaka mamlaka hiyo kuongeza kasi katika utendaji ili kufikia viwango vya juu zaidi ya ilipofikia sasa. Katika kufikia malengo hayo, Majaliwa aliiagiza TCAA kuimarisha mifumo ya udhibiti wa matumizi mabaya ya viwanja kwa kuhakikisha havigeuki kuwa uchochoro wa kupitisha bidhaa haramu.

Kwa kuweka msisitizo juu ya jambo hilo, Majaliwa aliitaka mamlaka kuhakikisha viwanja vilivyoko nchini, usalama unaimarishwa na haviwi uchochoro wa usafirishaji bidhaa haramu ili Tanzania iendelee kuwa na sifa kati ya nchi zenye udhibiti wa usafiri wa anga.

Aidha, Waziri Mkuu alibainisha kuwa Tanzania bado ina idadi ndogo ya marubani, hivyo kuiagiza Bodi ya Mkopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESL) kurejea mfumo na taratibu zake ili kuona uwezekano wa kutoa mikopo kwa vijana wenye uhitaji wa kusomea fani hiyo.

Kwa mujibu wa Majaliwa, gharama za kusomea masomo ya urubani au fani za masuala ya anga katika vyuo vya ndani na nje ni kubwa, hatua ambayo inawafanya Watanzania wengi kushindwa kuzimudu na kwamba kama kutakuwa na mikopo, ni dhahiri Watanzania watachangamkia fursa hiyo.

Mambo hayo mawili kati ya mengi aliyoyagusia katika maadhimisho hayo, ni ya msingi na kama yatatekelezwa vyema, ni wazi kwamba Tanzania itakuwa moja na nchi za viwango vya hali ya juu katika tasnia ya usafiri wa anga.

Suala la usalama katika viwanja vya ndege ni la muhimu kwa sababu litasaidia kudhibiti utokaji na uingiaji wa bidhaa haramu na za magendo kama vile dawa za kulevya na bidhaa hatarishi ikiwamo kemikali.

Miaka ya 1990 Tanzania ilijulikana duniani kama njia ya kupitishia bidhaa haramu na dawa za kulevya kutokana na baadhi ya abiria waliokuwa wakisafiri na mashirika kadhaa ya ndege za nje, walikuwa wakikamatwa kwenye viwanja vikubwa hasa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam na Kilimanjaro (KIA).


Watu kadhaa waliokamatwa na kufanyiwa operesheni waligundulika kuwa wamemeza pipi za mihadarati kama Cocaine na Heroine matumboni mwao.


Kwa ujumla, hatua hiyo ilipaka tope Tanzania kimataifa na kuonekana kichaka cha kupitishia au kuingizia dawa za kulevya. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, hali hiyo imebadilika baada ya kuimarishwa kwa usalama na kuwekwa mashine za kisasa zenye kubaini tishio lolote au kitu cha hatari kinachoingizwa au kutolewa kutoka nchini kwenda nje.

Kama alivyosema Mkurugenzi wa TCAA, Johari Hamza, kuwa wameendelea kuimarisha ulinzi, inatakiwa jitihada zaidi ziongezwe ili kutimiza azma hiyo kwa sababu ya mabadiliko ya teknolojia yanayotokea kila uchao duniani. Hiyo ina maana kwamba kadri teknolojia inavyokuwa, ndivyo wahalifu wanavyobuni mbinu mpya, hivyo hakuna budi kuongeza kasi katika kuimarisha usalama kwenye viwanja vya ndege nchini.

Kuhusu marubani, suala hilo pia linapaswa kuzingatiwa kwa sababu hivi sasa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeanzisha kozi za urubani, hivyo wigo zaidi unapaswa kupanuliwa ili kupata wataalamu wengi watakaofanya kazi kwenye ndege za ndani ili kupunguza tatizo la ajira na kuipaisha Tanzania kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Tuntule Swebe

## Muungwana Lazima Nilonge

# Elimu, nishati mbadala itaokoa mazingira

**UFUMBUZI** wa kupata nishati safi ya kupikia na kuachana na kuni na mkaa ili kulinda mazingira ni jambo linalohitaji kupewa msukumo mpya ili kuleta mabadiliko na kuondokana na upepo, jua na joto kali karibu kila mkoa.

Ni kipindi ambacho kuna jua kali na sehemu kubwa ya Tanzania inapitia kiangazi ambacho kinaambatana na upepo ambao licha ya kuchangia kukausha ardhi, maji na mazao pia kinafanya watu wasijisikie vizuri kiafya.

Ninachotaka kusema ni kuhimiza matumizi ya nishati salama kama gesi ili kulinda misitu na kuimarisha hali bora ya ikolojia.

Matumizi ya kuni kupikia si salama kwa mazingira hasa nyakati hizi za mabadiliko ya tabianchi yanayotishia hatma ya vitu vingi mijini na vijijini.

Ni wazi kuwa wakati huu watu wengi wana hofu baada ya taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa kutabiri mvua za eli-nino zinazoweza kusababisha maafa makubwa.

Tatizo mojawapo linaloongeza maafa kama el-nino, vimbunga, ukame, joto na upepo wa muda mrefu ni matumizi ya nishati chafu hasa kuni na mkaa zinazoleta zaidi joto kwenye uso wa dunia.

Mathalani mwaka 2018, Waziri January Makamba, wakati huo akiwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), alidokeza kuwa asilimia 70 ya wakazi wa Dar es Salaasm, bado wanaendelea kutumia tani nyingi za mkaa na kuni.

Licha ya kuwa kuna umeme wakati wote hali hiyo imeendelea kuwapo hata sasa, wengi wanategemea mkaa na kuni wawe mama lishe, hoteli, kwenye baa, shuleni, vyuoni na nyumbani.

Kutumia kuni kunamaanisha kuwa itafika siku mkaa na kuni vitamalizika kwa vile vinatokana na ukataji miti ambako ndiko kuondoa misitu.

Ukataji miti unatishia uhai wa viumbe vyote na ustawi wa sekta nyingi kama vile kilimo, upatikanaji wa maji, maisha ya mifugo, wanyama pori na kuongezeka joto zaidi.

Miti au misitu ni kila kitu kwa sababu mvua inatokana na misitu na hiyo ndiyo chanzo ya hewa inayohimilika kwa viumbe wote, inavyotoweka ndivyo nchi inavyogeuka jangwa, njaa kuongezeka, ukosefu wa maji na malisho ya mifugo na wanyama pori pia ukizidi.

Pamoja na upungufu huo ni wazi uzalishaji viwandani nao utakuwa kwenye changamoto kwa kuwa rasilimali za viwanda kuanzia za vyakula, mifugo hutegemea kilimo na misitu kwa kiasi kikubwa.

Ukweli ni kwamba kuendelea kucheza na mazingira kutasababisha uchumi kuyumba kutokana na misitu kukatwa hovyo kunakochangia baadhi ya wanyama kufa kwa kukosa chakula na makazi.

Kuendelea kukata na kuchoma moto mimea kuna uwezekano wa baadhi ya mitidawa na matunda ambacho ni chakula kutoweka.

Ni wakati wa kushirikiana na wadau kuendeleza matumizi ya gesi na nishati nyingine salama kama bi-ethanol, mkaa mbadala unaotokana na mimea na mabaki ya ya taka za nyumbani na viwandani.

Wakati wa kufuatilia na kuona mabadiliko kwa sababu hata watumishi wa serikali nao wanakuwa mstari wa mbele kubeba mkaa wanapotoka safarini.

Kwa mfano magari ya umma yanaonekana yakiingia mijini na magunia au viroba vya mkaa, ni vyema watumishi wa umma wawe mwanzo wa mabadiliko.

Si hao tu, wasomi wa vyuo vikuu na taasisi za elimu inashangaza mpaka sasa wanaendelea kutumia mkaa na kuni badala ya kuwa chachu ya mabadiliko na mwanga kwenye upatikanaji wa nishati mbadala.

Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ishirikiane na wadau wa ndani na nje kuwafikishia watu gesi pamoja na elimu kuhusu matumizi ya nishati mbadala.

Serikali pia iangalie uwezekano wa kupunguza gharama za gesi kama lengo namba saba la maendeleo endelevu ya dunia linavyoelekeza ili wananchi wenye kipato cha chini waweze kumudu kwani walio wengi wanaiogopa kwa vile wanajua ni vigumu kupikia vyakula vigumu kama maharage, makande na chakula cha watu wengi.

Wapewa elimu na nishati mbadala kuanzia mkaa, mafuta, bi-ethanol na ufahamu zaidi wa matumizi ya majiko banifu yanayotumia mkaa au kuni kidogo lakini yakipika kwa ufanisi.

Elimu pia iwafikie wanaouza nishati iwe gesi, mkaa mbadala wakihimizwa kujaza kwa kipimo sahihi ili kuepuka gharama zisizo za lazima kwa wateja ikiwezekana vipimo viandaliwe kwa uwazi sahihi kama kilo au lita na ithibitishwe na wataalamu wa vipimo.

HABARI KITAIFA

## PPRA yaokoa bil 2.6/- zilizochepushwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), imesema imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 2.6 zilizokuwa kwenye hatari ya kupotea kupitia mchakato wa ununuzi usiozingatia sheria na taratibu.

Pia, imesema imepata hasara ya Sh. bilioni 8.77 kutokana na kutokuzingatiwa kwa sheria ya ununuzi.

Meneja Uhusiano kwa Umma PPRA, Zawadi Msalla, alisema hayo hivi karibuni mjini Morogoro wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo katika kongamano la wahariri wa vyombo vya habari na wakuu wa vitengo vya mawasiliano na masoko kutoka kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha.

Msalla alisema fedha hizo zimeokolewa baada ya kufanya uchunguzi maalumu na zote zilizookolewa zitarudishwa serikalini kwa ajili ya matumizi mengine.

"Fedha hizo zimeokolewa baada ya mamlaka kufanya uchunguzi maalumu katika baadhi ya taasisi na tayari serikali imeshauriwa hatua za kuchukua dhidi ya wahusika ili kukomesha vitendo hivyo vinavyoligharimu taifa," alisema Msalla.

"Kuanzia mwakani PPRA itakuwa inawasilisha ripoti kwa Rais kama inavyofanya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na TAKUKURU."

Kuhusu mfumo mpya wa usimamizi wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST), Msalla alisema tayari umekamilika na kuanza kutumika tangu Julai, mosi mwaka huu.

"Hivi sasa kwa mujibu wa maelekezo ya mlipaji mkuu wa serikali kwa taasisi za umma, michakato yote ya ununuzi wa umma inafanyika kupitia mfumo wa NeST pekee kuanzia Septemba mosi mwaka huu,"alibainisha Msalla.

## BoT: Upatikanaji fedha za kigeni kuendelea kuimarika

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu (BoT), imesema hali ya upatikanaji wa fedha za kigeni inatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na matarajio ya mapato yatokanayo na shughuli za utalii, uuzaji wa madini, mazao ya biashara pamoja na hatua zinazochukuliwa na benki hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Gavana wa BoT, kamati hiyo imebaini uhaba wa fedha za kigeni ulioonekana hivi karibuni nchini umeendelea kupungua kutokana na ongezeko la mapato shughuli hizo za utalii, mauzo ya dhahabu na mazao ya biashara nje ya nchi.

Pia, alisema uuzaji wa fedha za kigeni uliofanywa na benki hiyo kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la mikopo inayotokana na uagizaji wa bidhaa nje ya nchi pia umesaidia kupunguza changamoto hiyo.

Kadhalika, alisema utekelezaji wa sera ya fedha nao umesaidia kupunguza shinikizo linalotokana na ongezeko la mahitaji ya fedha za kigeni nchini.

"Utekelezaji wa sera ya fedha, sera za kibajeti na kimfumo, zimesaidia kukabiliana na shinikizo la mfumuko wa bei, kuchangia ukuaji wa shughuli za kiuchumi na uhimilivu wa sekta ya fedha nchini licha ya mtikisiko wa kiuchumi duniani," ilieleza taarifa hiyo.

BoT ilisema kuwa katika kutathmini ya mwenendo wa uchumi nchini, kamati ilibaini kuwa Pato la Taifa kwa Tanzania Bara lilikuwa kwa kiwango cha kuridhisha cha asilimia 5.4 na asilimia 5.2 katika robo ya kwanza na ya pili, mtawalia huku kukiwa na matarajio ya kufikia makadirio ya ukuaji wa asilimia 5.3 kwa mwaka huu.

Kwa Zanzibar, ilisema uchumi ulikua kwa asilimia 6.2 katika robo ya kwanza ya mwaka huu na kukiwa na uwezekano wa kufikiwa kwa lengo la ukuaji wa asilimia 7.1 kwa mwaka huu.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya kuboresha mifumo ya masoko ya kilimo nchini (AMDT), Charles Ogutu (kushoto), akizungumza na mkulima wa mahindi katika bonde lililoko Kata ya Endiamtu, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Bryson Mbuya (kulia), wakati wa ziara ya kutembelea shamba la mfano la zaidi ya hekari 10 baada ya kupatiwa mafunzo ya upandaji wa mahindi na maharage kipindi cha kiangazi kwa njia ya umwagiliaji wa maji ya kisima. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Agro Tanzania inayofadhiliwa na ADMT katika kuwasaidia wakulima, Flora Marere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Washtakiwa wa kusafirisha nyara za serikali waongezewa mashtaka

**Na Kulwa Mzee**

WATUHUMIWA 11 wa kampuni wanaokabiliwa na mashtaka ya kusafirisha nyara za serikali zenye thamani ya Sh. bilioni 3.3 bila kibali, wameongezewa shtaka la kusafirisha vipande 1,107 vya mifupa ya simba.

Awali, walishtakiwa kwa kusafirisha kucha na meno ya simba na vipande 166 vya meno ya tembo.

Washitakiwa hao walibadilishiwa hati ya mashtaka juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mary Mrio.

Wakili wa Serikali, Neema Moshi aliwataja washtakiwa kuwa ni Abdulah Hamad, Kampuni ya AB Marine Products Ltd iliyopo Ubungo Maziwa, Roseline Wandera, Kennedy Mwambeta na Noel Kasaro.

Wengine ni walinzi wawili wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Tito Mwabe na Erasto Makinda, Theresia Lukanga, Abubakari Pazi, Haipeng Guo, Yassir Husein, Peter Kikweka.

Shtaka lililoongezwa ni kusafirisha mifupa ya simba vipande 1,107 na thamani ya nyara wanazodaiwa kujihusisha nazo kuwa ni Sh. 3,346,909,639.2 badala ya Sh 3,285,870,600 zilizokuwa zikidaiwa katika mashtaka ya awali.

Wakili wa Serikali Neema Moshi akiwasomea hati mpya ya mashtaka, alidai kati ya Januari mosi, mwaka 2019 na Mei 27, mwaka 2023 katika uwanja wa Ndege wa Pemba na Cabo Delgado Province, nchini Msumbiji, washtakiwa waliongoza genge la uhalifu kwa kupokea, kuuza na kusafirisha vipande 166 vya meno ya tembo vya thamani ya Sh. 3,285,870,600 Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Msumbiji, bila kuwa na kibali kutoka kwa Wakurugenzi wa Wanyamapori.

Katika mashtaka mengine wanadaiwa kupatikana na meno hayo ya tembo 20 na kucha 65 za Simba na vipande 1,107 vya mifupa ya simba bila kuwa na kibali.

Inadaiwa kuwa Mei 27, mwaka 2023 katika eneo lisilojulikana nchini Msumbiji, kwa nia ovu, washtakiwa walighushi nyaraka ya ubebaji mizigo na cheti cha afya, wakionyesha kuwa nyaraka hizo ni halali na zimetolewa na Mamlaka ya Wanyamapori ya Msumbiji, Jambo ambalo walijua kuwa sio kweli.


Pia, wanadaiwa kughushi nyaraka ikionyesha kuwa Mamlaka ya Wanyamapori ya Msumbiji imeruhusu kusafirisha samaki aina ya kaa wakiwa hai kutoka nchini humo kwenda Kuala Lumpur Malaysia, kupitia uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) uliopo Dar es Salaam.

Wakili Moshi alidai mshtakiwa Hamad na Kampuni ya AB Marine Products Ltd, kati ya Machi 28, mwaka 2021 na Machi 27, mwaka 2023 katika eneo la Mabibo, walijipatia nyumba moja wakati wakijua kuwa fedha za ununuzi wa nyumba hiyo zinatokana na zao la kosa tangulizi la kughushi nyaraka na kupatikana na nyara za serikali.

Baada ya kusomwa mashtaka hayo, upande wa mashtaka ulidai, haujakamilisha upelelezi wa kesi hiyo na aliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa na kupangwa Novemba 13, mwaka huu.

Washtakiwa wote walirudishwa mahabusu wakisubiri kuomba dhamana Mahakama Kuu yenye mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Chalamila: Gharama kupangisha vibanda Mwenge kuendana na hadhi

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema gharama zilizotumika katika ujenzi wa Soko la Mwenge ni kubwa na bei ya upangishaji wa vyumba vya biashara italingana na hadhi ya eneo na soko hilo.

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya waliokuwa wafanyabiashara wa eneo hilo kabla ya kujenga majengo mapya na stendi ya kisasa, wakitaka kupewa kipaumbele na wengine wakilalamika bei kubwa iliyopangwa.

Chalamila alisema, ujenzi wa soko hilo unafikia takribani Shilingi bilioni tisa na asilimia 60 ya vyumba vya biashara vimekwishapangishwa, akisisitiza kunahitaji kuwapo biashara za kisasa.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC) na kuelezea masuala mbalimbali ya mkoa huo, changamoto, mafanikio na matarajio.

"Jengo limegharimu takribani Shilingi bilioni tisa halafu leo mfanyabiashara aseme kwa sababu alikuwapo pale aje apange kwa kodi ndogo hii (hakutaja kiasi) si sawa, lazima tuambiane ukweli.

"Yaani tumpangishe mtu katika jengo la kisasa kwa kodi ya Sh. 100,000 halafu jirani kuna majengo ya watu binafsi tena ya kawaida kodi Sh. 1,000,000 kwa mwezi!

"Hadi sasa jengo limekwishajaa kwa asilimia 60 mtu ametoa pesa yake kodi ya mwaka mzima, tutaweka wapangaji wanaomudu gharama, lakini pia kukidhi gharama za uendeshaji na zilizotumika kujenga," alisisitiza Chalamila.

Alisema kwamba pia eneo hilo linahitaji kupanuliwa na kwamba zipo nyumba ambazo zimejengwa katika eneo hilo la serikali ambazo zitaondolewa na kuwataka wamiliki wake wajiandae kwa hatua za serikali.

"Mwenge ni eneo la serikali utashangaa mtu anasema ni eneo lake! kuanzia Mwenge hadi kilipo kituo cha mafuta kama unaelekea kituo cha daladala mpakani ni eneo letu, pote hadi kwenye Soko la Mwenge. Tunahitaji kupanua eneo la Mwenge," alisema Chalamila.

Hatua nyingine za mkoa alisema ni kupeleka mapendekezo kwa Wizara ya Nishati, kuufanyia ukarabati mfumo wa umeme soko Kuu la Kariakoo, ambalo linahitaji mfumo bora kwa usalama wa mali na biashara na taa katika kila mtaa, ili kuimarisha ulinzi wa biashara ya 24 itakayoanza.

Alisema mapendekezo hayo ya ukarabati mfumo wa umeme Kariakoo yanafikia Shilingi bilioni nane na pia ujenzi wa soko jipya na soko la zamani, umefikia asilimia 90 na gharama ni takribani Sh. bilioni 28 ambazo zitatumika hadi kukamilika kwa ujenzi wa masoko hayo.

"Tunahitaji kufanya ukarabati wa njia za umeme ili mfumo ukae sawa si kila mfanyabiashara kupitisha nyaya kiholela. Soko hili ni la kimataifa na tunataka kulifanya kuwa miongoni mwa maeneo ya biashara yanayofanya biashara kwa saa 24, lakini hii itakamilika kwa kuhakikisha uwapo wa taa kwenye kila mtaa," alisema Chalamila.

Alisema Mkoa wa Dar es Salaam ni kitovu cha pekee umeme unatumika takribani megawati 516 na kunahitajika uwekezaji wa uhakika hususan wa nishati hiyo ili kuongeza ufanisi wa shughuli za kiuchumi mkoani humo.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Mkoa wa Lindi, Twaiba Mpako, akihutubia mkutano wa vijana wa chama hicho tawi la Mnyangara-Mipingo, Jimbo la Mchinga mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha uhai wa jumuiya mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Dereva bodaboda apotea, familia yabaki njia panda

**Na Elizabeth Zaya**

ARAFAT Abdallah (23), mkazi wa Tabata mkoani Dar es Salaam, amepotea kwa muda wa zaidi ya mwezi mmoja sasa.

Akizungumza na mwandishi wa Nipashe huku akitiririkwa na machozi mama mzazi wa kijana huyo, Janeth Ndiyishao, alisema mwanawe alipotea tangu Septemba 15, mwaka huu.

Alisema mwanawe ni dereva wa pikipiki na alipotea siku ya tatu baada ya kuingia mkataba wa kazi hiyo na mmiliki mpya wa kifaa hicho cha kazi.

"Mwanangu kwa muda fulani alikuwa hana boda ya kufanyia kazi. Lakini bahati nzuri alipata nyingine ya mkataba na baada ya kusaini na kuanza kazi ndani ya siku tatu ndipo akapotea na hatujampata mpaka leo," alisema Janeth.

Alisema siku aliyopotea alikwenda na mwenzake kituoni kuweka mafuta na baada ya hapo alimuaga kwamba anakwenda nyumbani kwake kupumzika kwa sababu alikuwa anasumbuliwa na jino.

"Tangu siku hiyo hajaonekana. Na nyumbani alikuwa anaishi na mdogo wake hata hiyo siku aliyoaga kwamba anakwenda kupumzika hakuonekana nyumbani," alisema Janeth.

Alisema hata simu yake ya mkononi haipatikani tangu siku aliyopotea na kwamba wamemtafuta sehemu mbalimbali ikiwamo kwa marafiki zake, ndugu na hospitalini bila mafanikio.

Alitaja namba ya RB ambayo walipatiwa baada ya kuripoti kituo cha polisi cha Urafiki kuwa ni MAG/CID/PE/75/2023 na kuomba kwa yeyote atakayemuona au kufanikisha kupatikana kwake atoe taarifa kituo chochote cha polisi au kuwasiliana nao kwa simu namba 0713 367998 au 0713828625.

# Moto ulivyoteketeza mali za wafanyabiashara

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MOTO uliowaka kwa zaidi ya saa tano umeteketeza jengo la stoo lililopo ghorofa ya pili katika Mtaa wa Karuta katikati ya Jiji la Mwanza pamoja na mali za wafanyabiashara walizokuwa wakitunza katika stoo hizo zikiwamo bidhaa za kielektroniki.

Moto huo unadaiwa kuibuka majira ya saa tatu asubuhi katika moja ya chumba cha stoo ya mfanyabiashara aliyetambulika kwa jina moja la Mama Riziki kisha kusambaa katika stoo nyingine zilizopo katika jengo hilo huku chanzo kikiwa hakijafahamika.

Kwa mujibu wa baadhi ya wafanyabiashara na mashuhuda wa tukio hilo,walianza kuona moshi ukitokea kwa juu na jitihada ya kuuzima moto huo zilianza huku wakisubiri msaada wa Jeshi la Zimamoto ili kudhibiti.

"Zimamoto walifika hapa wakiwa na gari moja ambalo hata hivyo halikuwa na maji ikabidi kusubiri gari la pili huku wakiendelea kutusaidia kuondoa baadhi ya mali zisiungue na baadaye ndipo yalifika magari mengine mawili yakawa yanasaidiana kuzima moto huu," alisema Abdukarim Amza, shuhuda.

Mfabiashara Emmanuel Bagamba, alisema kuwa katika stoo hizo wafanyabiashara wengi wenye maduka wanahifadhi bidhaa zao ikiwa ni pamoja na redio, televisheni, magodoro na bidhaa nyingine.

Moto huo ulifanikiwa kuzimwa majira ya saa 8.30 mchana baada ya Zimamoto kupata msaada wa gari Mamlaka ya Viwanja vya ndege Nchini (TAA), magari ya majisafi kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania (JWT), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Mwanza (MWAUWASA) pamoja na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto Mkoa wa Mwanza, Mrakibu wa Zimamoto (SF) Kamila Labani, alisema moto huo ulianzia vyumba vya juu na kuudhibiti licha ya kuteketeza mali zote za wafanyabiashara zilizokuwamo ndani ya stoo hizo.

"Vitu vilivyokuwa vikiungua katika moto huu ni vyenye asili ya plastiki ndio maana hatua za kuzima zimechukua muda mrefu na kuwaka kwa haraka na kasi kubwa kwa ujumla hali sasa ni salama kwani kinachoendelea ni kuzima bidhaa za plastiki zilizopo chini ambazo kwa kawaida huchelewa kuzimika," alisema SF Labani.

Aidha, aliwataka wananchi kutoa taarifa za kutokea kwa moto mapema kabla hawajaanza shughuli za kuuzima kwa kuwa moto kwa bidhaa za plastiki unachukua muda mchache kusambaa ukicheleweshwa kudhibitiwa. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Wilbroad Mutafungwa, alisema jeshi hilo limedhibiti hali ya ulinzi na usalama wa watu na mali zao katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kusaidiana na Zimamoto.

"Tumesambaza askari katika eneo hili lote na kuhakikisha mali zilizookolewa zipo katika hali ya usalama na baada ya tukio hili polisi kwa kushirikiana na Zimamoto tutaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha moto huu," alisema SACP Mutafungwa.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi alitoa pole kwa wafanyabiashara wote ambao bidhaa zao ziliteketea katika moto huo huku akiwataka kuwa wavumilivu huku vyombo vya sheria vikiendelea na uchunguzi wa tukio.



## Wananchi wadai kufidiwa eneo la makazi

**Na Dege Masoli,** KILINDI

BAADHI ya wakazi wa Wilaya za Handeni na Kilindi, mkoani Tanga, wanaodaiwa kujenga nyumba za makazi na kuendesha shughuli za kiuchumi kwenye eneo la Hifadhi ya Msitu wa Bondo, wameiangukia serikali, wakitaka kufidiwa eneo jingine, badala ya kuondolewa kwa nguvu.

Tayari, serikali imeshatoa ilani ya kuwataka wananchi hao kuhama eneo hilo ili kupisha shughuli za uhifadhi kuendelea.

Kwa nyakati tofauti jana na juzi, wakazi hao wamepaza sauti kupitia vyombo vya habari, wakimuomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuelekeza halmashauri za wilaya hizo, kutafuta na kugawa ardhi nyingine kwa wakazi hao ili wapishe shughuli za uhifadhi kwa hiari.

Mmoja wa wakazi hao, Abdallah Mwebondo, alisema Wakala wa Misitu Nchini (TFS), imewataka kuyahama makazi yao, kwa kuwa wamevamia eneo la hifadhi, jambo ambalo limewachanganya.

"Kama ni eneo la hifadhi, mbona serikali ilishatujengea shule katika Kitongoji cha Bondo? Tena kwa kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo ya Ustawi kwa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambazo zilitolewa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Mwebondo.

Aidha, Herman Martine, alimuomba Rais kuingilia kati kero hiyo ikiwemo kuwasaidia eneo mbadala la kuishi kwa kuwa mpaka sasa hawana sehemu ya makazi mapya.

Naye, Joyce Nsavi, alisema hawapingani na serikali kuhusu kuondoka, lakini wanacholalamika ni kuondolewa kinyama na ndiyo sababu nao kuwa miongoni mwa wanaopata huduma za serikali kama vile shule.

Mohamed Alli, alidai kuwa wananchi hao wameishi katika maeneo hayo kwa zaidi ya miaka 40, lakini kwa hatua ya TFS kuwapa muda wa wiki mbili kuhama ni kuwanyima haki na kutaka kuwadhalilisha na familia zao.

Alipoulizwa kuhusu madai hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Hashim Mgandilwa, alisema tatizo hilo limesababishwa na viongozi wa vijiji, kuuza maeneo bila kufuata utaratibu, kanuni na sheria za ardhi.

"Tatizo ni viongozi wa serikali za vijiji kuuza maeneo hayo kwa wananchi huku wakijua kwamba ni eneo la Hifadhi ya Bondo," alisema.

# Mkutano wa kimataifa kamisheni ya misitu, wanyamapori wafanyika nchini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TANZANIA imeandika historia ya kuandaa kwa mara ya kwanza mkutano wa kimataifa wa Kamisheni ya Misitu na Wanyamapori Barani Afrika, ambao umeanza jijini hapa, ukiwashirikisha wajumbe 40 kutoka mataifa mbalimbali.

Wanaoshiriki mkutano huo wa 24 ni Mawaziri wa Maliasili na Utalii, Wakurugenzi wa Sekta za Misitu na Wanyamapori.

Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Kamisheni ya Misitu na Wanyamapori Barani Afrika, Prof. Dosantos Silayo, alisema lengo la mkutano huo ni kutoa fursa ya kubadilishana uzoefu wa usimamizi wa rasilimali za misitu na wanyamapori, kuweka mikakati ya pamoja ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

"Sekta ya misitu na wanyamapori inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, hivyo nchi zetu za Afrika zinapaswa kuweka mpango mkakati kwa kuwa rasilimali hizi zinavuka mipaka na changamoto zake zinavuka mipaka.

"Pia tumeweka mpango mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, masuala ya ujangili, uvunaji wa misitu usiozingatia sheria, changamoto za moto kwenye maeneo ya hifadhi na kilimo," alisema.

Alisema pia watajadiliana fursa za kibiashara zinazotokana na rasilimali kwa kuwa rasilimali ni jambo moja, lakini lazima zichangie kwenye maendeleo ya nchi.

"Matumizi sahihi na endelevu ya rasilimali hizi ni moja ya jambo tutakalojadili, pia masuala yanayohusu sera kwa kuwa rasilimali hizi zinategemea sera zilizoko na zinazotumika," alisema.

Aidha, Waziri wa Maliasili na Utalii, Angelah Kairuki, alisema mikutano hiyo imekuwa ikifanyika tangu mwaka 1960 na mwaka huu kwa mara ya kwanza kwenye mkutano wa 24 nchi ya Tanzania imekuwa mwenyeji na muandaaji.

"Kwa kweli ni heshima kubwa na tunashukuru kwa kuwa kati ya nchi 53 ambazo ni wanachama wa kamisheni hii tayari nchi 40 zimeshatuma wawakilishi wake na wengine tunatarajia wataendelea kuja," alisema Waziri Kairuki.

Kadhalika, alisema hadi sasa kuna washiriki zaidi ya 300 na wengine wanaendelea kuja, pia wako wanaoshiriki kupitia mitandao ya kidijitali.

"Nimepata nafasi ya kupitia progamu ilivyopangwa ni matumaini yangu wataalamu wetu kutoka serikali walioshiriki kwenye mkutano huu watanufaika kwa kuwa wataongeza ujuzi na maarifa," alisema Waziri Kairuki.

Ofisa Mkuu wa Misitu na Wanyamapori kutoka Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), Ofisi ya Afrika, Edward Kilawe, alisema kazi yake ni kuzisaidia nchi zote za Afrika ambazo ni mwanachama wao.

"Mkutano huu unawakutanisha wakuu wa misitu na idara za wanyamapori kwa nchi wanachama kwa ajili ya kujadiliana namna ya kuzinyanyua sekta hizi, kuangalia changamoto mbalimbali, kushirikiana na kubadilishana uzoefu kwa mambo yanayotokea ili kuwa na agenda ya pamoja kwenye mikutano ya kimataifa," alisema.



Mtendaji wa Mamlaka ya Mji wa Muheza, mkoani Tanga, Johari Mtango (kushoto) akiwazuia watoto na watu wazima kuvuka Mto Amtico katika eneo la Kwamtiga, Kata ya Genge, baada ya maji yake kufurika na kusambaa kwenye makazi ya watu kutokana na mvua kubwa iliyonyesha wilayani Muheza jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# IAA yazindua kamati maalum ushauri kisekta kuboresha elimu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA), kimezindua kamati maalum ya ushauri wa kisekta, ambayo itakuwa na jukumu la kushauri namna ya uboreshaji wa elimu na utekelezaji wa miradi chuoni hapo ili iendane na mahitaji ya jamii.

Akizungumzia umuhimu wake kwa wakati huu, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la IAA, Dk. Mwamini Tulli, alisema ujio wa kamati hiyo, utasaidia kuboresha elimu na kujenga ushirikiano na uhusiano wa karibu, kati ya chuo hicho na wadau kwenye sekta mbalimbali.

Alisema mradi huo, ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2021, unatarajiwa kukamilika mwaka 2026.

"Tunazindua kamati hii ya ushauri wa kisekta ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa HEET kwa lengo la kujenga daraja la kudumu kati ya chuo na wadau wetu katika sekta mbalimbali ambazo zitapokea wataalamu ambao tunawaandaa katika fani mbalimbali ikiwamo ya uhasibu, fedha, kodi, benki na utalii," alisema.

Aliipongeza serikali na Benki ya Dunia (WB), kwa kutoa fedha za uboreshaji wa miundombinu ya elimu kupitia mradi wa kitaifa wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi (HEET).


Mkuu wa Chuo cha IAA, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema tukio hilo ni mojawapo ya mpango wao ikiwamo kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu na kufanya utafiti.

"Majukumu haya hayawezi kwenda bila ya kuwapo kwa uhalisia wa kutoa majibu ya maswali yanayotokana na changamoto zinazotokea katika jamii kwa kutokuwa na mwongozo thabiti wa kufanya hivyo.

"Kuwapo kwenu hapa itakuwa ni kiunganishi kati ya sisi chuo na sekta na tunatarajia baada ya kamati hii kuanza kufanya kazi mtatupa mrejesho na miongozo ambayo itatusaidia kufanya vizuri," alisema Prof. Sedoyeka.

Alisema chuo hicho kimebahatika kupata mradi wa HEET na kilipatiwa fedha Dola za Kimarekani milioni 21 zaidi ya Sh. bilioni 45.

"Kuundwa kwa kamati hii ni hatua ya utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa umeelekeza kuhakikisha vyuo vinajengewa uwezo na kujipanga kutoa mazao bora ambayo yanaendana na mahitaji soko," aliongea.





# Wanufaika TASAF wapanda miti 4,000 kulinda mazingira

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MITI 4,000 imepandwa na wanufaika 56 wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Zahanati ya Masabi iliyopo katika Halmashauri ya Msalala, kwa lengo la kudhibiti mmomonyoko wa udongo na kupata kivuli kwa ajili ya wajawazito wanaofika kliniki.

Wanufaika hao kutoka kijiji cha Mega, Kata ya Masabi walipanda miti hiyo katika eneo lenye ukubwa wa hekta 3.5, ikigharimu Sh. milioni 30.5 fedha ambazo zimejumuisha malipo ya walengwa Sh. milioni 7.92 pamoja na fedha za vifaa wakati wa upandaji.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Masabi, Zephrine Mayani, ambaye ni msimamizi wa shamba hilo la miti alibainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari.

Walitaka kujua wanufaika wa TASAF wanavyoshiriki shughuli mbalimbali za kijamii na kuchagiza maendeleo katika vijiji, kata hadi wilaya.

Alisema, miti hiyo inatarajiwa kuwa mlinzi wa ardhi ya eneo la zahanati hiyo dhidi ya athari za mmomonyoko wa ardhi pamoja na uhifadhi wa mazingira kutokana na eneo hilo kuwa wazi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Msabi, Hassani Mayala alisema, jukumu lao kama serikali ya kijiji ni kuendelea kuitunza ili kutowavunja nguvu walengwa wa TASAF waliyoipanda, na kuhakikisha malengo yao ya kuona wajawazito wanapumzika eneo hilo wakisubiri huduma ya kliniki linatimia.

Alisema, wameweka makubaliano na wafugaji pamoja na wapita njia, kuwa atakayebainika kuchunga mifugo katika shamba hilo faini yake ni Sh. 5,000 kwa kila mfugo.

Akizungumza kwa niaba ya walengwa wa TASAF, Fortunatha Shija, alisema pia wamewanufaisha kwa kulipwa ujira wa Sh. 3,000 kila siku kwa muda wa siku 10 na fedha hizo ziliwasaidia kuongeza kipato katika familia yao, na kuahidi kuendelea kuwa watunzaji wa miti hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, tuzo ya kumpongeza Rais Samia kwa niaba ya wanawake wote wa mkoa huo jana, kutokana na utendaji kazi wake mzuri na kuiletea nchi maendeleo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Meya awaibukia madiwani wanaokwamisha maendeleo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MEYA wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, amewataka madiwani kuacha tabia za kukwamisha shughuli za kimaendeleo kwa kigezo cha kulinda kura kwa kuwanyima watendaji ushirikiano na kusababisha shughuli za ukusanyaji mapato kukwama.

Alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha kuwasilisha taarifa za utendaji kazi kwenye kata zao kuwa kumeibuka tabia baadhi ya madiwani kuwakwamisha utendaji kazi watumishi wa halmashauri kwa maslahi yao binafsi.

"Hii lugha ya kuwalinda wapiga kura acheni mara moja, tuna miradi mingi ya maendeleo ambayo inahitaji pesa hivyo naombeni muwape ushirikiano, suala la uchaguzi haliingiliani na kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya watumishi wetu," alisema Masumbuko.

Pia aliagiza moja ya kero ambayo iliibuliwa na Diwani wa Mwamalili Peter Kisandu, kuhusu baadhi ya wagonjwa waliojiunga na Mfuko Bima iliyoboreshwa (CHF) kutokuonekana katika mfumo na kukosa matibabu, ishughulikiwe haraka pamoja na kuendelea kuhamasisha wananchi wajiunge na bima hiyo.

Katika hatua nyingine Meya akiendelea kujibu kero ambazo zimetajwa na madiwani kwenye kata zao, likiwamo tatizo la kukithiri wizi shuleni zikiwamo mali za shule pamoja na masufuria ya kupikia chakula wanafunzi, aliagiza uanzishwe ulinzi shirikishi kwa kila eneo ili kulinda mali hizo.

Awali, Diwani wa Kata ya Kambarage, Hassan Mwendapole, alitaja kero za wizi shuleni kuwa zimekithiri kwa kuiba hadi vyombo vya kupikia chakula cha wanafunzi, na kuomba suala hilo lifanyiwe kazi ili kudhibiti wizi huo unaorudisha nyuma maendeleo.

Miongoni mwa kero zilizowasilishwa katika baraza hilo ni pamoja na ubovu wa miundombinu ya barabara, ukosefu wa maji, umeme, upimaji viwanja, upungufu matundu ya vyoo shuleni, maghuba kukithiri uchafu, upungufu watumishi na majina kutoonekana kwenye mfumo wa CHF.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Alexius Kagunze, alisema kuwa kero zote zilizowasilishwa na madiwani kwenye baraza hilo zitaendelea kutatuliwa.

# Wadaiwa kutumia muda wa masomo kuchota maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UKOSEFU wa huduma ya maji Kata ya Mondo Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga umetajwa kuwa kero kwa wananchi na chanzo cha idadi kubwa ya wanafunzi kukosa masomo yao na kutumia muda mrefu kufuatilia huduma ya maji yanayodaiwa kutokuwa safi na salama katika visima vilivyopo nje kidogo na kata hiyo.

Inadaiwa kuwa wanafunzi hao huamka alfajiri na kuelekea visimani kwa ajili ya kuchota maji ya matumizi ya familia na wakirejea nyumbani muda wa kwenda shule unakuwa umeinda na kusababisha utoro shuleni.

Hayo yalibainishwa juzi na diwani wa kata hiyo, Kija Peja, wakati akichangia hoja ya maji katika kikao cha kawaida cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2023 cha Baraza la Madiwani la manispaa hiyo.

Alisema kuwa katika kata kuna bomba la maji ya Ziwa Victoria lililopita kwenye eneo hilo kuelekea Nzega mkoani Tabora, lakini hawana maji na kuwa kero imewasilishwa muda mrefu katika mamlaka husika na ofisi ya Mkurugenzi.

"Hii hali imekuwa haivumiliki kwani utoro shule umekuwa ukisababishwa na adha hii, watoto wetu wa kike wanapoingia hedhi inawalazimu kusubiri mpaka muda upite ndipo waendelee na masomo kwani hata shuleni huduma hii hakuna," alisema.

Aidha, alisema kwa sasa wananchi wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 12 majira ya alfajiri kutafuta maji katika kata za jirani za Mwendakulia, Kagongwa na Kata ya Isaka hali inayohatarisha usalama wao na ndoa kuvunjika na huambatana na watoto wao ambao ni wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Diwani wa Kata ya Kahama mjini, Hamidu Juma, ambaye alisema kama bomba kubwa la maji ya Ziwa Victoria limepita ndani ya kata hiyo na kuelekea kata za jirani za Kagongwa na Isaka, kwanini wakose maji huku kata hizo wananchi wakipata maji.

Akijibu hoja hiyo kwa niamba ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA), Ofisa Mahusiano, John Mkama alikiri kuwapo kwa taarifa ya kata hiyo kukosa mtandao wa maji ya uhakika na kuendelea kutumia maji ya kwenye visima vilivyopo pembezoni na kwamba wanatafuta bajeti ya kutatua tatizo hilo kwa kushirikiana na RUWASA.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Clemence Mkusa alisema, ofisi yake inalifuatilia suala la ukosefu wa maji kuona ni jinsi gani ya kuhakikisha yanapatikana ili kunusuru wananchi na magonjwa ya mlipuko kwa kutumia maji machafu, kuyaelekeza shuleni ili kunusuru wanafunzi kuendelea kukosa masomo kipindi cha hedhi..



Ukurasa 12

**Miaka mitatu ikulu yashuhudia Rais Mwinyi akitakatisha ardhi**



Ukurasa 13

Ziara Rais Steimeier inavyoibua matumaini lukuki kwa Songea




Ukurasa 14

**Ushindi wa Tulia IPU ulivyo karata muhimu kidiplomasia**

siasa

JUMATANO NOVEMBA 1, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# Ndivyo Jaji Warioba anavyotamani ukomo wa mjadala katiba mpya

• Awanyooshea kidole wanaoukwamisha

**Na Sabato Kasika**



Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Jaji Joseph Warioba. **PICHA: MTANDAO**

MJADALA wa katiba mpya umedumu kwa miongo mitatu, lakini hata sasa bado kada mbalimbali zinatoa maoni kuunusuru mchakato wa kupata katiba hiyo uliosimama baada ya Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014.

Katika kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na ITV jana, Jaji Joseph Warioba, anatoa ya moyoni akijadili, anachoamini kinatakiwa kufanywa ili kufikia mabadiliko ya katiba Watanzania wanayoitamani.

Anakumbusha kuwa mjadala huo ulianza tangu mwaka 1992 ukiongozwa na vyama vya upinzani wakati wote, na kwamba kuna haja ufikie kikomo kusudi mambo mengine ya maendeleo yafanyike.

Anafafanua kuwa baada ya mjadala huo Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, akaona umuhimu wa kuwa na utaratibu wa mchakato wa mabadiliko ya katiba, akiunda tume ya mabadiliko ya katiba, ikiongozwa na Warioba, iliyozunguka Bara na Visiwani kupata maoni ya wananchi na kutengeneza kile kilichoitwa rasimu ya kwanza na kujiridhisha kwamba yale ambayo waliyapata kwa wananchi, yameingia kwenye rasimu.

Baadaye anasema tume ilirudisha rasimu hiyo kwa wananchi, katika mabaraza yao, waiangalie kama maoni waliyatoa yamezingatiwa na kwamba kiwango kikubwa walikubali kuwa maoni yao yameingizwa kwenye rasimu.

Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo ya Jaji Warioba na ITV

SWALI: Kwa sasa kinachozungumzwa sana ni uchaguzi, tume huru ya uchaguzi, kila wanasiasa au baadhi ya wanaharakati wazungumza kuhusiana na hilo. Kwa nini hasa?

JIBU: Tukifanya mabadiliko, lazima tufanye yote, kwenye rasimu yetu, ule mfumo wa uchaguzi, mapendekezo yale hayakuwa na matatizo kwenye bunge maalum, hayakupishana sana na maoni ya wananchi, lakini hili linazungumzwa kwa sababu inaonekana mabadiliko hayatakuja mapema kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025. Kwa hiyo wanasiasa ndio wanaona hili kwao ndilo muhimu zaidi, kwamba ibadilike. Si mbaya lakini ninasema hata wakibadili itakuwa inafuatana na mapendekezo yale yaliyokuwa kwenye rasimu ya tume pamoja na katiba inayopendekezwa.

SWALI: Kinachoonekana kwa sasa baadhi ya watu wanazungumza ni hata katiba iliyopo, baadhi ya wananchi hawaielewi, tume yenu ilitembea nchi nzima kukusanya maoni, wananchi hawana uelewa wa masuala ya katiba?

JIBU: Wana uelewa wa kila sheria, tunazo sheria nyingi sana, ukichukua sheria za haki jinai, zinahusu sana wananchi, hawazijui, lakini wanajua yaliyomo na wanajua wajibu wao, haki zao kwa sheria hizo. Sheria chukua mahali popote, kuna sheria nyingi sana ... na hata ya katiba, ni kweli wengi na sio wananchi wa kawaida tu, hata hawa viongozi, sio wote wanaijua katiba. Nilikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali miaka 10, nilikuwa ninahudhuria vikao vya viongozi iwe halmashauri kuu au bunge, ilikuwa ni kawaida kuniuliza katiba inasemaje? Ni viongozi hao, wanaapa kuilinda lakini sio lazima wajue kila kipengele. Lakini wanajua kwa kiwango nini katiba inataka. Kwa hiyo wananchi wengi hawajui lakini haki zao wanajua, maana ukienda kuwaelimisha juu ya katiba ya 77, utawaelimisha, lakini hayo ambayo wanataka hayamo katika katiba ya 77. Ninazungumzia mambo ya maadili, ukienda kuwafundisha ya katiba ya 77 hayamo. Sina hakika kama wote wanaosema wanataka katiba mpya wanaelewa iwe na nini. Maana inawezekana ni mambo ya uchaguzi.

Ndio maana ninasema wakati mwingine hatutazami nchi, tunajitazama, kwa hiyo vyama vinajitazama na kujitazama kwenye wananchi, wanaona ni mambo gani muhimu.

Na mimi kwa kweli kwa historia ambayo tumekuwa nayo ya mambo haya, Muungano miaka yote unazungumzwa, wananchi hawajui mambo muhimu ya Muungano? Wanajua, kwa hiyo mimi ninasema elimu tuitoe, lakini kuna umuhimu wa kushughulikia mabadiliko makubwa ambayo yamekuwa na mjadala kwa miaka 30.

Nafikiri hata tukienda kwenye uchaguzi wa mwaka 2025, kampeni itakuwa ni mabadiliko ya katiba. Ninapenda kampeni iwe ni ya maendeleo, tulimalize hili la katiba ili tuelekeze nguvu zetu zote kwenye maendeleo.

SWALI: Serikali imeshatangaza kwamba itatoa elimu ya katiba kwa miaka mitatu, ukiwa mbobezi wa masuala ya sheria, miaka mitatu inatosha kutoa elimu kwa Watanzania?

JIBU: Mafunzo ya sheria ni mazuri na yangekuwa kwa muda wote. Tuyaweke kwenye mitaala shuleni yafundishwe ili wanafunzi wajue misingi ya katiba, hakuna mtu ambaye anaweza kufahamu kila kipengele cha sheria, lakini wajue misingi yake, kwa sababu hiyo sina matatizo, lakini sio kusema kwamba ukienda uwape elimu ndio wanaweza kushiriki vizuri kwenye mabadiliko ya katiba.

Wamekwishashiriki, matatizo tunayafahamu yako wapi, katika kubadili katiba, nimeyataja hayo, ni sehemu inayohusu maadili, mgawanyo wa madaraka, mfumo wa uchaguzi na Muungano. Hayo ndio mambo makubwa ambayo ni lazima tujadiliane tufikie uamuzi, tukubaliane, lakini viongozi wakae na kazi ya kuonyesha utofauti ni rahisi sana.

Ukichukua katiba ya 77, rasimu na katiba iliopendekezwa utaona tofauti ziko wapi na kwa bahati, maana tume ilitoa mapendekezo mengi ilitoa rasimu, randama inayoeleza maana na kila kifungu, ikatoa na bango ambalo linaeleza kwa nini badiliko hilo limependekezwa na maoni ya wananchi yalikuwaje.

**INAENDELEA UK. 12**

# Miaka mitatu ikulu yashuhudia Rais Mwinyi akitakatisha ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MIAKA mitatu ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, tangu kushika usukani inatimia mwezi huu.

Ni kiongozi, aliyefanya mengi na mafanikio yameanza kuonekana katika kujenga misingi imara ya demokrasia, utawala bora, kukusanya mapato na kuimarisha uchumi.

Kazi zake zimewagusa wengi na hivi karibuni Waziri wa Ardhi na Makazi Rahma Kassim Ali, anazungumzia mafanikio ya miaka mitatu kwenye sekta hiyo.

Rahma anasema Rais anatambua na kudhihirisha kuwa ardhi ni muhimu kwa kila raia kwa sababu binadamu anapozaliwa anatakiwa kuishi sehemu salama na si kwingine ni juu ya ardhi hivyo, anaipa umuhimu wa kipekee.

Anaeleza kuwa pia ina umuhimu wake na ndiyo maana hata viongozi na waasisi wa Tanzania akiwamo Mwalimu Julius Nyerere, alisema vitu vitatu ni msingi wa maendeleo akitaja ardhi kuwa msingi wa maendeleo.

Katika kutekeleza majukumu ya kuboresha ardhi, hayo ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Dk Mwinyi, wizara imeanzisha mahakama ya ardhi ambacho ni chombo kipya cha kutoa haki akisema hapo awali hakikuwepo.

Anasema kipo kwa lengo la kusuluhisha na kutatua migogoro ya ardhi na kwamba katika uongozi wa Rais Mwinyi mahakama imefanya kazi zinazoweza kuthibitika.

Rahma anataja idadi ya migogoro 324 ya ardhi iliyotatuliwa kupitia mahakama hiyo, akisema katika kesi 521 zilizowasilishwa mahakamani 324 zimetatuliwa na kupatiwa ufumbuzi akiita ni hatua nzuri kwa sababu ya kushughulikia malalamiko mengi ya wananchi. Anasema kwa upande wa wizara pia husikiliza malalamiko ya wananchi kuhusu migogoro ya ardhi na kwa muda wa miaka mitatu imepata ufumbuzi wa migogoro 200 kati ya 380 iliyowasilishwa wizarani kwake.



Waziri wa Ardhi na Makazi Rahma Kassim Ali akizungumzia miaka mitatu ya uongozi wa Dk Mwinyi na mapinduzi sekta ya ardhi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Waziri Rahma anasema japo katika kutatua migogoro ya ardhi huchukua muda mrefu kutokana na wananchi kushidwa kukabaliana nayo kwa haraka kwa sababu ya umuhimu wa ardhi, lakini wizara husuluhisha na kutoa ushauri na wakishindwa kukubaliana huwapeleka mahakamani kwa ajili ya kutafuta haki zaidi.

Aidha, anasema kwa upande wa utambuzi wa ardhi, kuna sheria ya utambuzi ili kumtambua mwenye milki na hata katika ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 imeleza kutambua shehia 15 na tayari wizara imeshatambua shehia saba na hilo limefanyika..

"Utambuzi unaondoa migogoro mikubwa kwa sababu mtu anakuwa ameshatambuliwa kuwa ndiyo mmiliki halali wa ardhi hiyo na katika hatua ya utambuzi wanawashirikisha wananchi wenyewe wa shehia ili kusaidia kuwatambua wenye maeneo hayo na baada ya utambuzi wamiliki hupewa hati ya utambuzi wa ardhi,"anafafanua Waziri.

Akizungumzia uhaulishaji wa ardhi ambao upo kisheria, anasema katika miaka mitatu wamefanikiwa kwa sababu awali ulikuwa ukisimamiwa na bodi ya uhaulishaji lakini kwa sasa wameiondoa ili kupunguza urasimu na shughuli za bodi zinafanywa na kamisheni ya ardhi.

Anaeleza kuwa hatua hiyo imepunguza gharama za upatikanaji wa hatimiliki ya ardhi kwa wananchi, ambapo uhaulishaji kwa mujibu wa sheria ni hatua ya kutoka umiliki kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

"Uhaulishaji upo kwa njia tofauti, aidha kwa kununua ardhi, au kupewa zawadi au urithi hivyo lazima ardhi hiyo ihaulishwe kisheria ili kupunguza migogoro," anasema.

Akizungumzia kuhusu upimaji na upangaji wa ardhi, ambalo ni suala muhimu kwa sekta ya ardhi ikizingatiwa kuwa ardhi ya Zanzibar imepimwa kwa asilimia 10 pekee kwa upimaji wa kawaida, na wizara imeanza mazungumzo na kampuni mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kazi hiyo ili ikamilike kwa haraka kupunguza migogoro ya ardhi, akitaja kuwa ni mafanikio kwa sekta hiyo.

Anasema upimaji utafanikisha kujulikana kwa maeneo maalum ya serikali ikiwamo ya kilimo, misitu, uwekezaji na kuwa na ya akiba kwa matumizi ya baadaye kwa maendeleo ya vizazi vijavyo.

Kadhalika baada ya upimaji huo kutakuwa na mfumo wa taarifa zote za utambuzi, upimaji na uhaulishaji ambapo mfumo huo ni wa kisasa baada ya kutafuta taarifa katika majalada au mafaili na sasa wanakwenda kidijitali.

Kuhusu makazi, Waziri Rahma anasema Shirika la Nyumba Zanzibar, limefanyia matengenezo majengo mengi ya serikali ambayo yamechakaa na kujenga nyumba mpya na ujenzi unaendelea eneo la Mombasa kwa Mchina na nyumba 72 zinajengwa.

Anasema wizara yake kupitia shirika hilo la nyumba imefanya mazungumzo na taasisi za kibenki pamoja na wawekezaji mbalimbali kukarabati nyumba za serikali ambazo ni za muda mrefu.

Anafafanua kuwa ni kwa njia ya kuingia ubia ili kuzifanyia matengenezo na kuimarisha makazi.

Anasema licha ya kodi za nyumba za serikali kuwa nafuu lakini kuna changamoto ya wananchi kutolipa akieleza kuwa mapato hayo yangewezesha kuzifanyia matengenezo.

Nyumba hizo ni pamoja na za Michezani ambazo zilijengwa na Rais wa kwanza wa Zanzibar Hayati Abeid Amani Karume.

Aidha, serikali imeweka maeneo mapya kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya biashara zikiwamo eneo la Kisakasaka, Fumba, Kiembesamaki kwa Unguja na Pemba ni Chakechake.

"Pia tunatarajia kujenga nyumba za bei nafuu ili wananchi wenye kipato cha chini waishi katika makazi bora. Ardhi yetu Zanzibar ni ndogo na idadi ya wananchi tupo milioni 1.8 kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi na watu wanahitaji makazi hivyo lazima kujenga gorofa ili kupunguza changamoto ya ardhi,"anasema Waziri Rahma.

Anazungumzia migogoro ya ardhi, akisema mingi ipo katika maeneo ya uwekezaji kwa sababu ndiko kwenye fedha, lakini wizara yake itaharakikisha upimaji maeneo yote ya uwekezaji ili kuiondoa na kumaliza shida za wavamizi katika maeneo hayo.

Rais Dk Hussein Ali Mwinyi, alikula kiapo cha kuiongoza Zanzibar Novemba 2 mwaka 2020 baada ya kushinda katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, akipambana na mgombea wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye sasa ni marehemu.

Baada ya kumalizika uchaguzi huo Dk Mwinyi aliunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) na kuendeleza maridhiano na umoja wa kitaifa kwa kumteua Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Makamu wake wa kwanza hadi alipofariki 2021 na nafasi yake ikishikiliwa na Dk. Othman Masoud.

## Ndivyo Jaji Warioba anavyotamani ukomo wa mjadala katiba mpya

**INATOKA UK. 11**

Baada ya bunge kumaliza kazi yake, baadhi ya wajumbe wa tume walitoa waraka ambao unaonyesha tofauti iliyopo kwenye rasimu na katiba pendekezwa. Kwa hiyo ni rahisi kujua masuala ambayo hasa ni ya kujadili, viongozi wakikaa na kukubaliana itakuwa rahisi, hakuna haja ya kuwa na ratiba ndefu.

SWALI: Mkwamo unatoka wapi hasa, kwa sababu tume ilizunguka nchi nzima?

JIBU: Kwa sababu ni mambo yanahusu uongozi, viongozi ni lazima wafikie mahali wachukue maamuzi mazito hata yanayowahusu. Ukiangalia Muungano hakuna tatizo, zamani kulikuwa na mgawanyiko, mtu wa bara akienda Zanzibar alihitaji pasipoti, walipoanza kufanya biashara, waliotoka Zanzibar walionekana kama wananyanyaswa, lakini hayo yote yameisha. Wananchi hawana mipaka, wanajua haki za uraia wao na wanafanya kila kitu hawagombani, husikii kuna mgogoro iwe kulima au kuanzisha kiwanda hakuna tatizo na hata kero ambazo zinawahusu, zinatokana na maamuzi ya serikali mbili hizi, wanafanya uamuzi yanakuja kuathiri wananchi.

Kwa wananchi Muungano ni imara, ni hapa juu ya madaraka ni nani anakuwa na madaraka yapi, Serikali ya Muungano inakuwa na madaraka yapi, ya Zanzibar inakuwa na yapi? Haya ni madaraka tu, sasa mkikubaliana haya muone mnavyokwenda, itakuwa rahisi kuamua ni muundo gani tunakuwa nao. Si kitu kipya, kwani Azimio la Arusha lilipoletwa si lililenga zaidi viongozi? Lakini viongozi hao hao, walichukua uamuzi, waliitazama nchi wakaona kama uongozi utaendelea katika hali hii, tunaweza kupata matatizo.

SWALI: Kwa sasa watu wajikite wapi katika mijadala inayoendelea kuhusu katiba, awali ulisema tangu miaka 30 iliyopita watu wanajadili katiba, lakini wapinzani ndiyo wamekuwa wakijadili, wananchi wajikite katika nini?

JIBU: Tumefanya maandalizi ya kutosha, kwanza kumekuwa na mjadala kwa zaidi ya miaka 30, ukichukulia suala la Muungano viongozi wanajua, ninadhani ni utaraibu wa kufikia maamuzi. Ni viongozi hao ambao wamegawanyika wengine kubadili katiba ni kutaka waingie madarakani, wengine mabadiliko ni kutaka kuhakikisha wanabaki madarakani. Wanajitazama wenyewe, wananchi wana mwelekeo wao, sasa tukae kama viongozi wao, tuzungumze tunaweza kuamua vipi bila kuweka mbele maslahi binafsi.

Matumaini yangu ni kwamba mwaka 2025 tuwe tumemaliza suala la katiba mpya tuzungumzie maendeleo si katiba. Suala la kufanya marekebisho kwenye katiba iliyopo linaweza kufanyika hata kabla ya katiba mpya, kwani katikati na baada ya uchaguzi kuna mambo mengi yanatokea, hivyo suala la mabadiliko ndani ya katiba na sheria ni muhimu.




Rais wa Ujerumani, Dk.Frank Steinmeier, akikaribishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

# Ziara Rais Steinmeier inavyoibua matumaini lukuki kwa Songea

**Na Gaudensia Mngumi**

RAIS Frank Walter Steinmeier wa Ujerumani karibu Tanzania. Kiongozi huyu yuko katika ziara ya kihistoria ambayo inarejesha umma kwenye harakati za kupigania uhuru zilizotokea miaka 116 iliyopita.

Ni vita vya Majimaji baina ya Jeshi la Ujerumani na wapigania uhuru wa Tanzania wa mkoa wa Ruvuma waliopigana kwa miaka miwili kupinga ukoloni wa Mjerumani kuvamia nchi yao.

Rais wa Shirikisho la Ujerumani, Steinmeier, kwa mujibu wa Sauti ya Ujerumani -DW, ametembelea maeneo ambayo wakoloni wa Kijerumani walifanya uhalifu na katika ziara yake hiyo ya siku tatu atafika Songea kukutana na Wanasongea wakiwamo wana familia walioathirika na vita ya Majimaji.

Songea inapewa jina hilo kwa heshima ya kiongozi wa enzi za vita vya Majimaji Chifu Songea Mbano, aliyepigana na Wajerumani kuanzia mwaka 1905.

Aliongoza mapigano kukataa utumwa na ukoloni kupinga kutumikishwa kwa nguvu na utawala wa Kijerumani, kuporwa ardhi yao na kushurutishwa kuyahama makazi yao.

DW inakadiria kuwa wana Songea takribani 300,000 walipoteza maisha yao katika vita hivyo ambayo viongozi wa vita hivyo wakiwamo makamanda walinyongwa kwa kitanzi cha kamba.

DW inasema waathiriwa wa unyanyasaji huo uliofanywa na utawala huo wa zamani wa kikoloni wa Ujerumani wanataka Rais Steinmeier ajumuike nao kuwakumbuka ndugu zao waliokuwa waathiriwa wa vita hivyo.

Hata hivyo kinachosisitizwa ni kuwa ni vizuri kuwa Steinmeier anafanya ziara hiyo lakini, ni lazima afike na majibu na kieleweke kwa kuwa kichwa cha Chifu Songea Mbano kilichukuliwa na mwili wake kuzikwa Songea.

Vita hiyo ya majimaji iliyopiganwa kuanzia mwaka 1905 hadi 1907, ni moja ya kazi za kishujaa zinazoiweka Tanganyika na Tanzania leo katika ramani ya dunia kwa kuwa makabila mbalimbali yalitumia silaha za jadi kupinga uvamizi wa majeshi ya kigeni.

Licha ya Mjerumani kuwa na silaha za kisasa, ujuzi na weledi kwa Wangoni walisimama kukataa ukandamizwaji wakitumia silaha ya umoja wao kumtetea mzalendo.

**KILICHOJIRI**

Mwanahabari Mwandamizi na Mwenyekiti mstaafu wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Ruvuma, Juma Nyumayo, anakumbusha kuwa katika mapambano hayo yaliyomalizika miaka 116 iliyopita, wapiganaji maelfu walinyongwa na kuzikwa katika kaburi la pamoja.

Lakini askari wa Ujerumani, walishindwa kumnyonga kamanda wa vita hiyo Chifu Songea Mbano, ambaye kamba ya kitanzi ilikatika zaidi ya mara tatu kila walipoanza kumnyonga.

"Iliposhindikana kumnyonga, walimpiga risasi na kukata kichwa wakakipeleka Ujerumani. Walimzika kwenye kaburi lake peke yake jirani na lile la pamoja lililokuwa la askari maelfu," anasema Nyumayo.

Baadhi ya wakazi wa Songea waliozungumza na Nipashe wanasema kuwa wana familia wa Chifu Songea Mbano, bado wana machungu kuhusu kuchukuliwa kichwa cha babu yao huyo na kuomba kirudishwe kizikwe nyumbani kwao.

Baadhi ya machifu walioshiriki vita hivyo ni pamoja na Zulu Gama.

Baltazari Nyamusya Mhifadhi wa Makumbusho ya Taifa ya Vita vya Majimaji, anapuzungumzia ziara hiyo ya Rais Steinmeier, anasema wanamkaribisha katika makumbusho yao ambayo ni pekee yenye uhifadhi wa historia ya uzalendo, mapigano ya kupinga ukoloni, ukandamizaji na dhuluma za ubeberu.

Makumbusho hiyo ina hadhi ya kimataifa na inatambulika na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ikiwa na zana za kihistoria kama mishale, mikuki (fumo), ngao na kaburi la pamoja la askari wapambanaji pengine zaidi watu 300,000 na kaburi la pembeni la Chifu Songea Mbano.

Akizungumzia ujio wa Rais wa Ujerumani, mwana ukoo wa Chifu Songea Mbano, Samuel Mbano ambaye ni diwani wa Kata Mshangano, anazishukuru juhudi za serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Ubalozi wa Ujerumani nchini kufikia hatua hiyo.

> "Aliongoza mapigano kukataa utumwa na ukoloni kupinga kutumikishwa kwa nguvu na utawala wa Kijerumani, kuporwa ardhi yao na kushurutishwa kuyahama makazi yao.

Anasema mambo mengi yamefanyika ikiwa ni pamoja na wanafamilia yao kuzuru Ujerumani kuomba kurudishwa nyumbani kwa kichwa cha babu yao Chifu Songea Mbano.

"Tumewasiliana na Balozi wa Ujerumani nchini amefika Songea, aidha taifa hilo limetuma timu ya watu 15 waliofika kutembelea na kuhakiki. Leo tunafarijika na ujio wa Rais Steimeier, tukiamini kuwa ni kufungua mlango wa ushirikiano baina ya Tanzania, Manispaa ya Songea na Ujerumani."

Akizungumzia baadhi ya mambo wanayotamani yakamilishwe na ziara hiyo kwenye ushirikiano Samuel anasema wangetamani Manispaa ya Songea na Ruvuma yenye maji ya kutosha.

Anakumbusha kuwa manispaa hiyo inakua na inaendelea kiuwekezaji na wanatamani kuwe na maji ikiwezekana kutoka Mto Ruvuma ili kumaliza tatizo hilo.

Aidha, Diwani anazungumzia kuponywa maumivu na kupata faraja kwa Ujerumani kujenga barabara za kuunganisha wilaya zote za mkoa huo kwa kiwango cha lami, kusaidia kuendeleza juhudi za uhifadhi na historia ya Tanzania kwa kujenga makumbusho hiyo kwa usasa na kuvutia zaidi.

Aidha, Samuel anautaja ujenzi wa shule au taasisi ya elimu kwa heshima ya Chifu Mbano itakayofundisha masuala mbalimbali ya historia, ushirikiano baina ya Tanzania, Afrika na Ujerumani, bila kusahau mafunzo ya sayansi na teknolojia.

# Ushindi wa Tulia IPU ulivyo karata muhimu kidiplomasia

**Na Mwandishi Wetu**

KUCHAGULIWA kwa Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Akson, kuongoza Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), kumetafsiriwa kama nafasi ya Tanzania kurejea kwenye ramani ya diplomasia ya kimataifa.

Historia inaonesha kuwa enzi za kupigania uhuru barani Afrika hadi miaka ya 90, Tanzania ilikuwa mshawishi mahiri kwenye medani za kidiplomasia kiasi cha mataifa yenye ushawishi kutamani kusikia msimamo wa Tanzania kwenye ajenda za kidunia.

Wachambuzi wa masuala ya siasa na utawala, wanaeleza kuwa kuchaguliwa kwake kunaimarisha uhusiano wa Tanzania kwenye anga za kimataifa kisiasa.

"Inarejea kwenye utukufu wake kama ilivyokuwa enzi za kupambana na kupinga unyonyaji, ubeberu na ubepari hali iliyoipa heshima zaidi duniani," ansema mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Abbas Mwalimu.

Mhadhiri huyo wa Chuo cha Salim Ahmed Salim, anasema kuchaguliwa kwa Dk. Tulia kuwa rais wa mabunge hayo, pia kunaleta ushawishi mkubwa kwa Tanzania kwa mataifa mengi duniani.

Anasema wakati ule Tanzania ilikuwa ikizungumza katika vikao vya baraza na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Muungano wa Nchi za Afrika (OAU), watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa mataifa makubwa duniani walikuwa wakisubiri kwa hamu kusikiliza nini kitatamkwa.

Anasema hata juhudi za ukombozi nchi za Kusini mwa Afrika chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kituo chake kilikuwa jijini Dar es Salaam kwa sababu Tanzania ilikuwa na ushawishi mkubwa kwa mataifa mbalimbali duniani kutokana na juhudi zake za kuhakikisha mataifa ya Afrika yanakombolewa kutoka kwa mabeberu.

Anasema wakati wa ukombozi wa nchi hizo, ikiwamo Msumbiji wakati ule ikiitwa Mozambique kutoka kwa Wareno, vikao vyake vilikuwa vikifanyika nchini kutokana na ushawishi wa Tanzania kwa mataifa makubwa duniani.

Vikao hivyo vilimshikisha kiongozi wa Chama cha FRELIMO, hayati Edward Mondlane kwa kushirikiana na Samora Machel na kupata mafunzo nje ya Msumbiji, namna ya kumfukuza mkoloni na kuiacha nchi hiyo huru.

Mwalimu anaenda mbali zaidi akisema kuchaguliwa kwa Dk. Tulia ni mkakati wa Tanzania kupenyeza ushawishi wa lugha ya Kiswahili kutumika katika vikao vya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Anasema hata katika IPU neno Bunge limeandikwa kwenye tovuti yake na kwamba hatua hiyo itayafanya mataifa mengine duniani kufahamu kuwa ni la Kiswahili na ni lugha ya taifa la Tanzania.

Anasema nafasi nyingine kubwa ambayo Spika huyo atakuwa nayo ni mshawishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Afrika.

Mwalimu alimpongeza Dk. Tulia kwa kushinda kwa kishindo katika uchaguzi huo kwa kupata kura 172.



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Akson. **PICHA: MTANDAO**

> Niwaombe linapotokea suala la kitaifa tuwe kitu kimoja badala ya kuungana na adui zetu kuumizana wenyewe kwa wenyewe.

"Ni mafanikio kwa nchi yetu na kwake mwenyewe kulingana na kura nyingi alizopata," anasema Mwalimu na kusisitiza kuwa:

"Ni namna gani Dk. Tulia anatumika kimkakati kukikuza Kiswahili, lengo letu ni kupenyeza ushawishi kama ilivyokuwa kipindi kile."

Kwa mujibu wa Mhadhiri Mwalimu, baadhi ya kura alizopata Dk. Tulia ameungwa mkono na nchi takribani 167 duniani.

Anataja baadhi ya nchi hizo kuwa kwa Afrika 52, Uarabuni 20, Asia Pacific 26, Urusi 10, nchi za Jumuiya ya Kikanda Afrika Magharibi (ECOWAS) 15 na za Amerika Kusini 26.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga anasema: "Ushindi wa Dk. Tulia ni jambo la kujivunia kama Watanzania, wanawake na Tanzania imetajwa kwa jina kubwa duniani."

Anasema Watanzania wanakila sababu ya kujivunia ushindi huo wa kishindo wa zaidi ya kura zaidi ya 100 na kuwabwaga wagombea wengine watatu.

Wagombea hao ni Adjiarra Kanote wa Senegal aliyepata kura 59, Catherine Hara wa Malawi (61) na Marwa Hagi wa Somalia (11).

Dk. Tulia, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, alichaguliwa kuwa Rais wa IPU Oktoba 27, mwaka huu katika uchaguzi uliofanyika jijini Luanda nchini Angola.

Dk. Tulia Ackson, anashika wadhifa huo baada ya mtangulizi wake, Spika wa Ureno, Duarte Pacheco kumaliza muda wake na kuwa Rais 31 wa IPU tangu kuanzishwa kwa bunge hilo.

Kwa kipindi cha miaka 25 iliyopita, marais wa IPU walikuwa ni kutoka mataifa ya Misri, Hispania, India, Chile, Italia, Namibia, Morocco, Bangladesh, Mexico na Ureno.

### KAZI YA TULIA IPU

Wachambuzi wa masuala ya kimataifa wanaeleza kuwa Dk. Tulia ana kazi kubwa ya kutafsiri kwa vitendo maono na dhamira ya IPU ndani na nje ya Tanzania.

IPU iliyoanza mwaka 1889 kama kikundi kidogo cha wabunge, kilichojitolea kukuza amani kupitia diplomasia ya bunge na mazungumzo, limekuwa na kuwa shirika la kimataifa lenye wanachama 180 na wanachama washirika 14.

Miongoni mwa majukumu ya IPU ni kuwezesha diplomasia ya bunge na kuwapa mabunge na wabunge uwezo wa kukuza amani, demokrasia na maendeleo endelevu duniani kote, ikitumia kaulimbiu yake ya 'Kwa demokrasia, kwa kila mt.'

Maono ya IPU ni kuona kila demokrasia ikishamiri kwa kuheshimu sauti za watu na mabunge yakihudumia watu kwa amani na maendeleo.

Dhamira ya chombo hicho chenye nguvu duniani, ni kukuza utawala wa kidemokrasia, taasisi na maadili kwa kushirikiana na mabunge na wabunge kueleza na kujibu mahitaji na matarajio ya wananchi.

IPU inafanyakazi kukuza amani, demokrasia, haki za binadamu, usawa wa kijinsia, uwezeshaji wa vijana, hatua za hali ya hewa na maendeleo endelevu kupitia mazungumzo ya kisiasa, ushirikiano na hatua za bunge.

Makao makuu ya IPU yako jijini Geneva, Switzerland, zikiwa na ofisi ndogo New York, Marekani na Vienna, Austria.

### DK. TULIA NA MASWAHIBU MITANDAONI

Dk. Tulia amerejea nchini juzi na kuzungumzia mbivu na mbichi alizopitia hadi kuchaguliwa kuwa Rais IPU kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Dk. Tulia ameeleza namna ambavyo mitandao ilitumika kufanya kampeni chafu dhidi yake, kwenye sherehe za kumpongeza kwa kuchaguliwa kushika wadhifa huo na kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika. Sherehe hizo zilifanyika kwenye viwanja vya Bunge, jijini Dodoma.

"Uchaguzi ule ulikuwa mgumu sana na hii ni kutokana na mitandao ya kijamii kutumika kunichafua. Tena waliofanya hivyo ni Watanzania wenzetu ambao walikuwa wanaungana na watu wengine ili tu nisishinde kwenye nafasi hii," anasema Dk. Tulia na kuongeza:

"Niwaombe linapotokea suala la kitaifa tuwe kitu kimoja badala ya kuungana na adui zetu kuumizana wenyewe kwa wenyewe."

Anasema makubaliano ya awali yalikuwa mataifa mengine ya nchi za Afrika yasiweke wagombea ili kuiunga mkono Tanzania, lakini kutokana na maneno ya mitandao ya kijamii, nchi nyingine zilipata nguvu ya kuingiza wagombea wao.

"Nchi nyingi zilisema hazitaingiza wagombea na kuipa nafasi Tanzania lakini sasa maneno ya kwenye mitandao yaliwapa nguvu ya kuleta wagombea...kwa kuwa Mungu alikuwa amepanga Tanzania ishinde, hakuna kilichobadili hilo," anasema.

Anasema watu waliokuwa wanaichafua Tanzania na mgombea wake, baadhi waliwahi kuwa viongozi ambao walishika nafasi katika nyadhifa za juu za kitaifa.

Dk. Tulia ambaye ni mwanamke wa pili kuongoza Bunge hapa nchini, anasema kila aliposemwa yeye huwa anafurahi, lakini kwa hilo huyo mmoja aliyeshiriki kumchafua, lazima amtafute kwa lengo la kujifunza kutoka kwake kwa kuwa hawezekani mtu aliyewahi kuwa kiongozi wa juu kitaifa kuungana na adui kuichafua Tanzania.

Anasema kuchaguliwa kwake katika kinyang'anyiro hicho kunatokana na kuungwa mkono na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kumpa kibali cha kuingia katika kinyang'anyiro hicho.

Anasema Rais Samia alikuwa mstari wa mbele kuitangaza diplomasia ya Tanzania kwa mataifa mengine na kushiriki kumpigia kampeni kwa mataifa mengine duniani ambayo ni wanachama wa IPU.

Anasema uamuzi huo wa Rais Samia uliwafanya baadhi ya wajumbe kuja wa IPU kufika na maagizo kutoka katika serikali za nchi zao.



## Madarasa yaongeza idadi ya wanafunzi kujiunga na masomo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UJENZI wa madarasa matatu pamoja na matundu mane ya vyoo Shule ya Wasichana ya Kondoa, umechangia kuongeza idadi ya wanafunzi kujiunga na shule hiyo kutoka 660 hadi 800.

Madarasa hayo na matundu ya vyoo yamejengwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu Sh. milioni 75.8 ambazo zitatumika kukamilisha ujenzi huo.

Akisoma taarifa ya mradi huo mbele ya madiwani wa Kamati ya Fedha na Utawala wa Halmashauri ya Mji Kondoa, Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Flora Nusu, alisema ujenzi wa madarasa hayo unakwenda kutatua changamoto za ufinyu wa vyumba vya madarasa, lakini utasaidia kuongeza udahili wa wanafunzi waliomaliza shule za msingi.

Aliishukuru serikali kwa kuwaletea fedha hizo ambazo zitakwenda kumaliza kero ya madarasa katika shule hiyo.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutupatia fedha hizo, tunaimani zitatusaidia kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo na matundu ya vyoo," alisema Nusu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji, Mohamed Kiberenge alisema wanajamii ni watu muhimu katika utekelezaji wa mradi huo, wanapaswa kujua kila kitu kinachofanyika katika mradi huo kwa kuwa ni wa kwao.

Wajumbe hao wamepongeza utekelezaji wa mradi huku wakishauri kukamilika kwa mradi kwa wakati ili utoe huduma kusudiwa kwa wananchi.

Alisema ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Bolisa umepata fedha Sh. milioni 544 kutoka Serikali Kuu huku majengo mbalimbali yanajengwa likiwamo jengo la utawala, maabara tatu, maktaba, jengo la ICT, madarasa matundu ya vyoo na sasa ipo katika hatua za ukamilishaji.

Katika hatua nyingine Kiberenge aliwataka walimu wa Shule ya Sekondari Kondoa kusimamia utekelezaji wa mradi wa ukarabati huo ili fedha zilizotolewa ziboreshe mazingira.

Alisema kuwa serikali imeona umuhimu wa kuleta fedha hizo na kutaka zitumike vizuri ili umuhimu wake uonekane.

**"Tunaishukuru sana serikali kwa kutupatia fedha hizo, tunaimani zitatusaidia kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo na matundu ya vyoo," alisema Nusu.**

# Watanzania watakiwa kuwekeza kwenye teknolojia ya akili bandia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Tehama nchini (ICTC) imesema kuna umuhimu wa Watanzania kuwa na ujuzi wa kidijitali ambao unaendeshwa na akili ya bandia (AI) ili kufanya uchumi kuwa wa ushindani.

Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Nkundwe Mwasaga, aliyasema hayo hivi karibuni katika kongamano la saba la Tehama lililokutanisha wataalamu wa ndani na nje ya nchi ili kupata uzoefu wa teknolojia zinazotumika kwenye mataifa mengine ikiwamo akili bandia ili kutengeneza ajira kwa vijana na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alibainisha kuwa zipo faida nyingi kuwekeza kwenye akili bandia ikiwamo kukuza uzalishaji na ufanisi na uchumi na ubunifu.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na McKinsey nchini Uingereza, inakadiriwa akili ya bandia inayozalishwa inaweza kuongeza pato la taifa la Uingereza kutoka Dola za Marekani trilioni 2.6 hadi 4.4 kwa kulinganisha, mwaka 2021 lilikuwa Dola trilioni 3.1.

Kadhalika, alisema Tume hiyo imeendelea kufanyia kazi kero zinazowakabili wanawake ili kuongeza ushiriki wao kwenye sekta ya Tehama ambayo ina fursa nyingi za kiuchumi.

"Lengo letu ni kujenga uchumi wa kidijitali ambao unawagusa watu wote tunachokifanya ni kuhakikisha zile nguzo tano za mapinduzi ya kidijitali zinaguswa kwa watu wote," alisema.

Alitaja nguzo hizo ni pamoja na kuwapa watu ujuzi, kuhakikisha mifumo salama inayoaminiwa, huduma za mawasiliano zinawafikia watu wote, kujenga uchumi wa kidijitali na ujasiriamali wa kidijitali.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akimwapisha Mbunge mpya wa Jimbo la Mbarali, Bahati Ndingo, katika mkutano wa 13 kikao cha kwanza cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC aagiza maDC kusimamia mbolea iwafikie wakulima

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba amewaagiza wakuu wa wilaya mkoani hapa kusimamia mbolea iliyotolewa na serikali kwa ajili ya msimu wa kilimo mwaka huu ili iwafikie wakulima wote kwa wakati na kusitokee hujuma yoyote.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa kongamano la uzinduzi wa msimu wa kilimo kwa mwaka 2023/2024 lililofanyika katika Wilaya ya Iramba, Mkuu wa mkoa alimwakilisha Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

"Ma-DC hakikisheni mbolea ya ruzuku iliyotolewa na serikali isimamieni kikamilifu na kuifikisha kwa wakulima wote hadi ngazi ya kata ili iweze kupatikana kwa urahisi kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa mafuta ya kula nchini na mazao mengine," alisema.

Serukamba alisema katika msimu wa kilimo wa 2022/2023, Mkoa Singida ulizalisha mafuta ya alizeti kwa zaidi ya asilimia 50 ambayo yanatumika nchini pamoja na mazao mengine ambayo yalipatikana mkoani hapa.

"Msimu wa kilimo uliopita tulifanikiwa kuzalisha vizuri mazao ya chakula na haukuwa miongozi mwa mikoa ambayo haikujitosheleza kwa chakula, hivyo nawaomba wakulima ongezeni kasi katika kilimo ili kwa msimu ujao wa 2023/2024 uzalishaji uweze kuongezeka hadi kufikia asilimia 80 na kujitosheleza kwa chakula," alisema. Alisema Mkoa wa Singida unajivunia kuwa miongoni mwa mikoa minne nchini ya kimkakati katika suala la uzalishaji wa mazao ya kilimo cha alizeti, huku ukipunguza nakisi ya mafuta ya kula na kupunguza kwa kiwango kikubwa matumizi ya fedha za kigeni ambazo hutumika kuagiza mafuta kutoka nje.

"Tumefanikiwa kutengeneza ajira zaidi ya vijana na wanawake katika sekta ya kilimo na mazao ya kilimo ambapo ukipita kandokando ya barabara kuu za mkoani Singida utashuhudia kinamama na vijana wakiuza mafuta ya kula, vitunguu, asali, kuku na mayai," alisema.

Serukamba alisema mkoa huo miaka 60 tangu uanzishwe haujawahi kufikiriwa kama ungeweza kuwa kati ya mikoa minne kinara katika msimu wa kilimo kwa mwaka 2022/23 kutokana na historia ya ukame.

Aliongeza kuwa kwa Wilaya ya Iramba imenufaika kwa kupata ruzuku ya mbegu ya alizeti aina ya Record tani 75 zenye thamani ya Sh. milioni 337.5, pikipiki 34 kwa ajili ya maofisa ugani kwenye kata zote 20 kwa ajili ya msimu huu wa kilimo.

"Mheshimiwa Rais ameleta mbolea ya ruzuku ambapo katika msimu uliopita Iramba ilisambaziwa tani 539 na mwaka huu mpaka sasa wakulima wa Iramba wameshasambaziwa tani 475 na kazi ya usambazaji inaendelea," alisema.





# Tisa familia moja washikiliwa tuhuma kumuua bibi wakimtuhumu ni mchawi

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WATU tisa wa familia moja wakazi wa Kijiji cha Mbembe, Wilaya ya Wanging'ombe, mkoani Njombe, wanashikiliwa na polisi mkoani humo kwa tuhuma za kumuua kwa kumpiga na kigoda kichwani Zainabu Mkupasi (78), wakimtuhumu kuwa ni mchawi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 28.

Alisema kabla ya kutekelezwa kwa mauaji hayo, wanafamilia ya mzee Mkupasi walishiriki kikao cha pamoja kilichojadili suala la ushirikina huku wakimtuhumu Zainabu ambaye ni mama wa familia hiyo.

Kamanda Banga alisema ili kukabiliana na matukio ya mauaji ya imani za kishirikina, jeshi hilo linaendelea kutoa elimu.

"Tunaendelea kutoa elimu kupitia wakaguzi wa kata, lakini bado tunaendelea kuhimiza viongozi wa dini, mashehe na wachungaji kuendelea kufanya taratibu za kiroho wanapokuwa katika ibada zao, kwamba wamuogope Mwenyezi Mungu na waepukane na matendo ya namna hiyo," alisema Banga.

Mkuu wa wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, alikemea vitendo vya mauaji akisema havivumiki na akithibitika mtu kukatisha uhai wa mwingine, vyombo vya ulinzi na usalama vitahakikisha vinakomesha matukio hayo.

"Hakuna mtu duniani hasa katika taifa letu la Tanzania katika mkoa wetu wa Njombe wilaya yetu ya Wanging'ombe hakuna mwenye haki ya kumuua mwenzake ili yeye aendelee kuishi, mwenzake awe kaburini awe udongo, hayupo kitendo hiki hakikubaliki," alisema Kitta.

Kitta, alisema hadi sasa wameshakamata watu wanane na upelelezi unaendelea ili kuwabaini wengine.

Diwani wa Kata ya Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa, alisema katika kijiji cha Mbembe kwa miaka minane sasa kumekuwa na mfululizo wa visa vya mauaji yakihusisha vikongwe kwa tuhuma za ushirikina na migogoro ya ardhi.

Nyagawa alitoa msisitizo kwa jeshi la polisi kukamatwa kwa watuhumiwa wengine ili kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kuwa matukio yaliyotokea awali hakuona mtu yeyote aliyekamatwa.



Baadhi ya wachimbaji wa madini ya dhahabu wakiendelea na shughuli ya kutakatisha dhahabu kwa kutumia zebaki ambayo inadaiwa kuwa ni hatari kiafya katika eneo la Itumbi, Kata ya Matundasi, wilayani Chunya, mkoani Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TAKUKURU kuelimisha vijana kutoa taarifa rushwa ya ngono

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Njombe, imesema imejipanga kuanza kutoa elimu kwa vijana wa kike kuvunja ukimya ili kutoa taarifa ya vitendo vya rushwa ya ngono mkoani humo.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa Uchunguzi Mwandamizi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Njombe, Daniel Mntambo, wakati akizungumza na Nipashe katika maonesho ya Viwanda Vidogo (SIDO), Mkoa wa Njombe.

Alisema kuwa kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2020, asilimia 34.4 ni vijana kuanzia miaka 15-35 na wengi wapo shuleni.

"Tumeamua kuwatafuta vijana mwaka huu kuanzia mwezi wa 11 hadi 12, tunataka tutembelee vyuo vyote vya Mkoa wa Njombe, huko tunataka tukafundishe wanafunzi," alisema Mntambo.

Alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwafanya wanafunzi kufahamu mambo ya rushwa.

"Kwanza wajue rushwa ni nini, lakini wakapambane na rushwa, vijana kwa upande wa jinsia ya kike wanahusishwa na rushwa ya ngono na inakuwa na pande mbili, kuna wakati wanafunzi wanawasumbua walimu halafu kuna walimu wanasumbua wanafunzi," alisema Mntambo.

Alisema kwa jinsia ya kike mwanafunzi hasomi, lakini anataka apewe alama kubwa.

Pia, Mntambo alitoa wito kwa wananchi kutoa taarifa ya vitendo vya rushwa kwa kutumia namba 113, na mtoa taarifa atalindwa kwa mujibu wa sheria.

# Sakata wakulima kakao kutolipwa fedha zao kitendawili

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SAKATA la viongozi wa vyama vya ushirika wa wakulima wa kakao wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya, kutafuna fedha za wakulima limeendelea kuwa kitendawili kwenye baadhi ya maeneo, wakulima wakidai hawajalipwa fedha zao licha ya mazao yao kuchukuliwa kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Hivi karibuni baadhi ya wakulima wa zao hilo waliomba serikali kuingilia kati wakidai kuwa mazao yao yaliuzwa kwa njia ya mnada, lakini fedha zao hawajalipwa na kuwa na wasiwasi ya kuingia hasara.

Baada ya malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliunda kamati maalumu ya kufuatilia sakata hilo na kubaini kuwa fedha za wakulima zaidi ya Sh. milioni 800 zilikuwa zimetafunwa na viongozi wa vyama vya ushirika kwa kushirikiana na watunza maghala.

Baada ya ripoti hiyo, Homera aliagiza viongozi wote wa vyama hivyo kukamatwa na kuswekwa ndani na akatoa siku 14 kwa viongozi hao kurejesha fedha za wakulima huku akisisitiza kuwa wasipolipa wataendelea kusota rumande.

Baada ya siku 14 kukamilika baadhi ya wakulima wamedai kuwa hawajalipwa fedha zao hali ambayo inawapa wasiwasi kuwa matamko yanayotolewa na viongozi wa serikali ni ya kisisasa na hayatekelezwi.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Mlaghila, maarufu Kinanasi, wananchi wa kata za Ikama, Makwale na Mwaya, walisema mpaka sasa hawajalipwa.

Mmoja wa wakulima hao, Ganon Mwakyeja, alisema kakao zao zilichukuliwa wakati wa mnada wa 10 uliofanyika Agosti, mwaka huu, lakini mpaka sasa hawajalipwa fedha zao hali inayosababisha maisha yao kuwa magumu.

Alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliagiza wakulima wambao mazao yao yanauzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi ghalani wawe wanalipwa fedha zao ndani ya saa 48 ili waone faida ya mfumo huo.

Alisema awali walipopeleka mazao yao waliamini utaratibu huo ungefuatwa, lakini mpaka sasa inakaribia kukamilika miezi miwili bado hawajalipwa na kumuomba mbunge wa jimbo hilo awasaidie kudai.

"Baada ya saa 48 tuliendelea kuwa wavumilivu, ikaisha wiki ya kwanza bado tukawa wavumilivu, lakini sasa ni zaidi ya mwezi, tunaomba utusaidie kulipigia kelele jambo hili ili tulipwe fedha zetu," alisema Mwakyeja.

Kenan Mwambambale, alisema baada ya Mkuu wa mkoa kuagiza walipwe ndani ya siku 14 waliamini kuwa wangelipwa, lakini mpaka sasa hali iko vilevile na hawajui hatima ya malipo yao.

Alisema kwa sasa wamekuwa wakikamatwa na maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na kutakiwa kila chama cha ushirika kuchangia magunia 20 huku wakiwa bado hawajalipwa fedha zao.

Alisema kwa sasa hawaelewi magunia wanayotakiwa kuchangia ni kwa ajili ya kazi gani na kumuomba mbunge wa jimbo hilo kuwasaidia kuwasilisha kilio hicho serikali kuu.

Akijibu kero za wakulima hao, Mbunge wa Jimbo la Kyela, Kinanasi aliwataka wakulima wa kakao wilayani humo kuungana kwa pamoja katika kupigania jambo hilo ili wapate haki yao.

Alisema wapo baadhi ya viongozi wamekuwa wakiwagawa wakulima hao na kuficha baadhi ya taarifa muhimu ili kupotosha uhalisia wa jambo hilo ambalo linawatesa wakulima.

Alisema atahakikisha anawasaidia wakulima hao kupata haki yao kwa kuwawasilisha kero zao serikali kuu ili kuhakikisha haki hiyo inapatikana haraka.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera alisema baada ya kuwakamata viongozi wa vyama vya ushirika waliokuwa wanatuhumiwa kutafuna fedha hizo, tayari wameshaanza kurejesha fedha hizo na wakulima wanaendelea kulipwa kwa awamu.

Alisema wakulima waliokuwa wanadai fedha zao walikuwa 572 na waliokwisha lipwa mpaka sasa ni wakulima 326 na wengine wanaendelea kulipwa.





## Makumbusho Visiwani, Bara kushirikiana uendeshaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDARA ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania Bara, zimetiliana saini hati ya ushirikiano wa usimamizi na uendeshaji wa makumbusho na maeneo ya historia ya pande hizo.

Akizungumza katika hafla hiyo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Naibu Katibu Mkuu wizara hiyo, Dk. Amina Ameir Issa, alisema hatua hiyo itasaidia kushirikiana pamoja katika shughuli mbalimbali kwa lengo la kuyaendeleza maeneo hayo.

Aidha, hatua hiyo itasaidia watendaji wa wafanyakazi wa taasisi hizo kutanua wigo kwa kushirikiana katika nyanja mbalimbali za kiutendaji na kuyatangaza maeneo hayo ndani na nje ya nchi.

Alisema, makubaliano hayo pamoja na mambo mengine pia yatatoa matokeo chanya kwa kuyaendeleza maeneo hayo kufanya utafiti na kuyahifadhi ili kukuza uchumi wa nchi hizo kupitia utalii wa urithi.

Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Marcelline Bernard Patrice, alisema hatua hiyo inakwenda sambamba na kutekeleza kwa vitendo, usimamizi na ushirikiano wa uendelezaji wa sekta ya malikale kwa sehemu mbili hizo.

Alisema kupitia hatua hiyo itatoa fursa ya kukuza sekta hizo katika nyanja mbalimbali ikiwamo utunzaji, utangazaji na maeneo mengine ili kunufaisha kizazi cha sasa na kijacho.

Mkurugenzi Mkuu Makumbusho ya Taifa Tanzania Bara, Dk. Noel Lwoga, alishukuru kukamilika mkataba huo kwasababu ushirikiano wa taasisi hizo ulianza zamani na shughuli mbalimbali zilikuwa zikifanyika, lakini haikuwa rasmi na kupitia hatua hiyo umeleta sura nyingine.

Alisema kupitia hatua hiyo itakuwa chachu ya kufanikisha uendeshaji wa maeneo hayo kwa kupatikana rasilimali mbalimbali ikiwamo fedha na mambo mengine kwa ajili ya kuyaendesha ili kuchochea uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar, Maryam Mohammed Mansab, alisema idara hiyo imeweka mikakati ili kuhakikisha sekta hiyo inaimarika na kuwa chachu ya kuleta tija nchini.

Alisema hatua hiyo ni moja ya kudumisha na kuendeleza muungano wa nchi hizo kwa lengo la kuona kila mmoja ananufaika na rasilimali hizo kwa maslahi mapana ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

Akizungumzia baadhi ya maeneo ambayo watashirikiana, alisema ni pamoja na uhifadhi wa kisayansi kwa mikusanyo ya makumbusho, uhifadhi wa majengo ya kale, usajili wa kidijitali kwa mikusanyo ya makumbusho na mambo ya kale, uandaaji wa matamasha na maonesho na maeneo mengine.

# Marekani yaingia ubia na ZAFICO kuimarisha sekta ya uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya Marekani (ZANFRESH), imeingia ubia wa uendeshaji wa shughuli za uvuvi wa bahari kuu Tanzania na kampuni ya uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ili kuimarisha sekta hiyo visiwani Zanzibar.

Mpango huo umeelezwa na Mkurugenzi Mwendashaji wa ZAFICO, Amiri Haidar Mshenga, alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu mwelekeo wa utekelezaji wa mpango wa uchumi wa buluu kupitia rasilimali za baharini ulioanzishwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, baada ya kuingia madarakani mwaka 2020.

Alisema kampuni ya ZANFRESH ina uzoefu wa kimataifa katika uvuvi wa bahari kuu na itachangia kwa kiwango kikubwa kuleta mageuzi ya kisasa na kuvutia wawekezaji wengine kutoka mataifa mbalimbali kuwekeza katika sekta hiyo.

"Bodi ya Wakurugenzi ya ZAFICO imepitisha mpango wa ubinafsishaji kwa kampuni ya ZANFRESH kutoka Marekani, mikataba tayari imeridhiwa baada ya serikali kupitisha mpango huo wa ubinafsishaji," alisema.

Alisema wataalamu kutoka ZAFICO na mamlaka ya usafiri wa baharini Zanzibar (ZMA) wanatarajia kuondoka mwezi huu kwenda kukagua meli ya kwanza ya uvuvi MV CUTETA, kabla ya kampuni hiyo kusajiliwa Zanzibar.

"Ukaguzi utafanyika nchini Senegal, lakini kampuni yenyewe inatokea Marekani kabla ya kusajiliwa Zanzibar na baada ya kukamilika ukaguzi itakabidhiwa bendera ya Zanzibar na mamlaka ya usafiri bahari ZMA na lengo la meli hiyo iwe imewasili Zanzibar Desemba, mwaka huu," alisema.

Alisema meli hiyo ni kubwa na ina kiwanda cha kuchakata samaki ndani na ZAFICO itanufaika na mambo mengi ikiwamo uzoefu na ujuzi wa wafanyakazi na ajira zitakazo jitokeza baada ya kampuni hiyo kuanza kazi rasmi.

Alisema kiwanda cha samaki kinatarajiwa kuanzishwa katika jengo la ZAFICO huko Malindi na kibali cha ruhusa ya kujenga upya jengo au kulifanyia matengenezo makubwa kimewasilishwa mamlaka ya uhifadhi mji mkongwe kabla ya hatua kuanza kufanyika.

Alisema hatua ya ubinafsishaji itasaidia wafanyakazi wa ZAFICO kupata ujuzi na uzoefu wa uvuvi wa bahari kuu kwa kampuni za kimataifa ambazo zimekuwa na uzoefu kwa muda mrefu katika shughuli za uvuvi wa bahari kuu.

"Mpaka sasa kampuni ya ZAFICO ina meli mbili za uvuvi changamoto kubwa uzoefu kwa wafanyakazi katika masuala ya uvuvi wa bahari kuu, nakumbuka tuliwahi kupoteza mtego mmoja wenye thamani ya Sh. milioni 110 baharini hatukuweza kuupata, lakini serikali imeshanunua miitego mipya na sababu kubwa ni ujuzi na uzoefu," alisema Mkurugenzi.

Alisema serikali imeamua kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya uvuvi kwa kushirikiana na sekta binafsi na tayari imetenga Sh. bilioni 34 kuimarisha miundombinu ikiwamo kujenga viwanda vya usarifu wa dagaa na kuchakata minofu ya samaki.

Alisema, serikali inajenga kiwanda cha kisasa cha kusarifu dagaa na minofu ya samaki katika eneo la Kama, Wilaya ya Magharib 'A' Unguja, kitakachonufaisha wavuvi kutoka maeneo ya wilaya hiyo ambacho kitakuwa na huduma za maduka 48, benki, nyumba za gharama nafuu kwa wajasiriamali na ujenzi umefikia hatua kubwa.

Alisema kiwanda kingine cha kusarifu dagaa kinatarajiwa kujengwa Fungu refu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, pamoja na kiwanda cha kuchakata samaki kitakachojengwa kwa kushirikiana na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo la Mkokotoni kupitia Mradi wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD).



Mwenyekiti wa Taifa wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Daktari wa Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe, Muhamed Juma Nahoda, katika ziara maalumu ya kutembelea miradi ya maendeleo Mkoa wa Kusini Unguja mwishoni mwa wiki. **PICHA: MAELEZO ZANZIBAR**

# CCM yajiwekea matumaini kushinda majimbo 50

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimesema kina matumaini makubwa ya kushinda majimbo yote 50 ya uchaguzi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kutokana na kazi kubwa inayoendelea kuonekana ya kuwasogezea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari wa CCM, Khamis Mbeto Khamis, alipokuwa akitoa taarifa ya kupongeza wagombea wote walioshiriki uchaguzi mdogo Jimbo la Mtambwe, katika mkutano na waandishi wa habari.

"Kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Dk. Mwinyi, ameonesha kutekeleza ilani ya uchaguzi vizuri mpaka sasa, wenye macho sote tunaona na wasio na macho wanasikia, ameweza kujenga hospitali kila wilaya, shule za kisasa za ghorofa na mji mzima umebadilika tukishuhudia barabara za ndani na barabara kuu zikijengwa ndani ya miaka mitatu ya uongozi wake, Zanzibar ya zamani sio ya sasa," alisema Mbeto.

Alisema wananchi wa Pemba wamebadilika kisiasa kwa kiwango kikubwa kutokana na maendeleo wanayoyashuhudia, pamoja na utulivu wa kisiasa hali ambayo imeondoa mazingira ya vitisho yaliyokuwa yametawala katika siku za nyuma za kusababisha wana CCM kugopa kuvaa sare zao.

"Jimbo la Mtabwe sio ngome ya upinzani tatizo watu walikuwa wakipata vitisho, lakini mabadiliko ya hali ya kisiasa yaliojitokeza CCM inamwelekeo mkubwa wa kuchukua majimbo yote uchaguzi ujao na sote tumeona kampeni za uchaguzi mdogo watu walivyojitokeza bila ya hofu, lakini hili pia limechangiwa na maendeleo wanayoendelea kuyashuhudia visiwani humo," alisema.

Aidha, alisema wapinzani ndani ya Baraza la Wawakilishi wana viti vinne vya uwakilishi katika majimbo na uchaguzi ujao CCM inaamini itashinda majimbo 50, lakini wagombea wote waliojitokeza katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mtambwe wanapaswa kupongezwa kwa kufanya kampeni za kistaarabu.

"Nawapongeza wagombea wote, lakini nimpongeze mshindi katika uchaguzi huo ingawa wenzetu walianza kuonesha wasiwasi kwa kuzungumza mambo mbalimbali jambo la msingi tumefanya uchaguzi kwa amani," alisema Mbeto.

Akijibu swali la hali ya ngumu ya maisha kutokana na mfumuko wa bei uliojitokeza visiwani humo, alisema tatizo hilo ni la kiulimwengu na limesababishwa na mambo mbalimbali ikiwamo athari ya maradhi ya corona yaliojitokeza, kupanda kwa bei ya mafuta tangu kuibuka kwa vita vya Urusi na Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo alisema kazi ya serikali ni kuimarisha miundombinu ya huduma za jamii na kazi hiyo inaendelea kufanyika ili kuharakisha maendeleo yatakayosaidia kujenga uchumi imara na hakuna serikali duniani inayompelekea mwananchi chakula nyumbani kwake.

Mbeto alisema katika kupunguza makali ya mfumuko wa bei, serikali imekuwa ikitoa Sh. bilioni 22 kufidia gharama za mafuta ili yasipande bei na kulinda sekta ya usafiri na uchukuzi katika juhudi zake za kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi huku mipango ya kuimarisha miundombinu kama ya bandari ikiendelea kufanyika na mizigo kutolewa kwa wakati.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

FOMU MIRATHI - 3

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 1432/2023**

**Jina la Mdai MUGEMANA JEAN BOSCO**

**Jina la Mdawia NDAYAHOZE FLORENTINE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA TALAKA**

Unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 14 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa 4:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh. MWAGENI kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 31 Mwezi 10 Mwaka 2023.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**CONSTANTINE NGERERY MBOWE** anatangaza kupotelewa kwa hati yangu ya kusafiria namba **TAE337345** iliyotolewa uhamiaji makao makuu mnamo tarehe 17/04/2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/MAG/19640/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**REBECCA LEONARD MWENGWA,** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Chuo Kikuu chenye namba za usajili **D210006** kilichotolewa na Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es salaam mwaka 2017, yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **PHQ/MBE/MBE/5094/2023.**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



MUNA ABDALLAH ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASIPOTI YAKE YENYE NAMBA TAE296072 ILIYOTOLEWA 05 FEB 20 NA MAMLAKA YA PCO DAR ES SALAAM

KWA ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KWA NAMBA PHQ/ARU/ARU/1/1855/2023.

## KUPOTEA KWA BARUA YA OFA

**DEMERE DYNESS KITUNGA,** (Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **CHACHAGE SEITHY LOTH CHACHAGE**), anatangaza kupotea kwa Barua ya Ofa ***(Letter of Offer of Right of Occupancy)*** yenye namba ya usajili **BAG/6604/3** ya Shamba Namba **2594**, liliopo Mapinga, Bagamoyo la Marehemu **CHACHAGE SEITHY LOTH CHACHAGE**.

Kwa yeyote atakayeona atoe taarifa Kituo cha Polisi au apige simu namba **0754 275 347**

**PHQ/DAR/KIN/29820/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN RICHARD SAFARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **GS GROUP LTD.** aina ya **HAOJUE** namba za usajili **MC865DXE.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/6001/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA LILILOPO BUKOBA, KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA. 91/2023**

**KAIGALULA BYASHALILA ..........................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **CHRISTOPHOLO BYASHALILA**
2. **SAMWEL RWEBANGIRA ................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: CHRISTOPHOLO BYASHALILA**
**SAMWEL RWEBANGIRA (POPOTE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na. 91/2023 yamepangwa kutajwa tarehe 06/12/2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, **P. J. MAKWANDI** saa 2:00 asubuhi. Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 19/10/2023.

..................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - BUKOBA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA LILILOPO BUKOBA, KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA. 103/2023 (Yatokanayo na Maombi Na. 91/2023 katika Baraza la Wilaya Bukoba)**

**KAIGALULA BYASHALILA ......................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **CHRISTOPHOLO BYASHALILA**
2. **SAMWEL RWEBANGIRA ...............WAJIBU MAOMBI**

**KWA: CHRISTOPHOLO BYASHALILA**
**SAMWEL RWEBANGIRA (POPOTE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na. 103/2023 yamepangwa kutajwa tarehe 06/12/2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P. J. MAKWANDI saa 2:00 asubuhi. Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 19/10/2023.

..................................
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - BUKOBA

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN RICHARD SAFARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **GS GROUP LTD.** aina ya **HAOJUE** namba za usajili **MC865DXE.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/6001/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......58/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: IDDY KIBANGULA IDDY WA KIHONDA -MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KIBANGULA IDDY SONGORO**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 02 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

**Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 10 mwaka 2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Wu_ haiming** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **PHOTON SEMI TALLER** yenye namba za usajili **T834DFS**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi: **PHQ/KIG/BUH/806/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSHUA YUDANI LUVANDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4213/0069** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MARIAN BOYS SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/32653/2023.**

***OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mob: +255 - 0677020701***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA, NA WENYE ULEMAVU**

## TAARIFA KWA UMMA

## TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KATIKA SEKTA ZA USAFIRISHAJI, TEHAMA, MADINI, KILIMO, UJENZI, UZALISHAJI, UBUNIFU WA MITINDO NA USHONAJI NGUO, HUDUMA ZA HOTELI NA UTALII

1. Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini inayowezesha nguvu kazi ya Taifa kupata ujuzi na stadi za kazi stahiki ili kumudu ushindani katika soko la ajira. Ofisi imeingia makubaliano vyuo mbalimbali kutoa mafunzo mafunzo ya ufundi stadi kukuza ujuzi na stadi za kazi kwa vijana. Miongoni mwa mafunzo yatakayotolewa ni Ubunifu wa Mitindo na Ushonaji Nguo, Ufundi Bomba, Uashi, Useremala, Uchomeleaji na Uungaji vyuma, Upakaji rangi na maandishi ya alama, Utengenezaji wa vipuri vya mitambo, Ufundi Magari na Mitambo, Umeme wa Majumbani na Viwandani, TEHAMA, Umeme wa Magari, Huduma za Hoteli na Utalii, Ukataji Madini ya Vito na Kilimo.

2. Hivyo, tunapenda kuwatangazia vijana wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 wanaopenda kujiunga na mafunzo katika mojawapo ya fani zilizoorodheshwa hapo juu wafike katika vyuo vilivyoainishwa na Tangazo hili hapa chini ili kuchukua fomu ya kuomba kujiunga na mafunzo. Serikali itafadhili ada ya mafunzo kwa asilimia 100. Mwanafunzi / mzazi / mlezi atagharamia gharama nyingine zikijumuisha nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani. Mafunzo yatakayotolewa ni ya kutwa hivyo mwombaji anashauriwa kuomba mafunzo haya katika chuo kilicho katika Mkoa anaoishi.

3. Maombi yawasilishwe kuanzia tarehe 01/11/2023 hadi tarehe 14/11/2023 yakiambatana na nyaraka zifuatazo:
   i. Barua ya maombi ya mafunzo;
   ii. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa;
   iii. Nakala ya Cheti cha elimu uliyohitimu ;
   iv. Kitambulisho cha uraia / kadi ya mpiga kura (Kwa wenye miaka 18 na kuendelea);
   v. Barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji anakoishi mwombaji; na
   vi. Picha nne za paspoti (ziandikwe majina matatu ya mwombaji kwa nyuma).

4. Sifa za kujiunga na mafunzo haya ni:
   i. Elimu ya msingi au zaidi kwa fani za ubunifu wa mitindo na ushonaji nguo, ufundi bomba, ujenzi, useremala, uchomeleaji na uungaji vyuma, upakaji rangi na maandishi ya alama;
   ii. Elimu ya kidato cha nne na kuendelea kwa fani nyingine zilizobaki zikijumuisha fani ya utengenezaji wa vipuri vya mitambo, ufundi magari, umeme wa majumbani na viwandani, TEHAMA, umeme wa magari na umeme wa jua (solar);
   iii. Awe Mtanzania;
   iv. Awe na umri kati ya miaka 15 – 35;
   v. Awe mwenye afya njema;

5. Vijana wa Kike na Vijana Wenye Ulemavu wanasisitizwa kuomba fursa hizi na watapewa kipaumbele katika nafasi za mafunzo haya;

6. Maombi yachukuliwe na kuwasilishwa kwenye vyuo vilivyo katika Mkoa wako ambavyo vimekubaliwa na Serikali kutoa mafunzo haya; na

7. Watakaokidhi vigezo na sifa tu ndio watakaochanguliwa

**Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Ofisi (www.kazi.go.tz)**

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MKUU**
**01/11/2023**

*NB: Fomu za maombi zinapatikana katika vyuo vyote vilivyopitishwa na Serikali kutoa mafunzo haya*

## VYUO VILIVYOKUBALIWA KUTOA MAFUNZO YA UANAGENZI

| NA | MKOA | WILAYA | JINA LA CHUO | FANI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Arusha Jiji | Don bosco KII - TECH | Umeme jua |
| | | | | ufundi umeme |
| | | Karatu | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mto wa Mbu | Uongozaji Watalii |
| | | | | Ufundi Bomba |
| | | | | Umeme wa Majumbani |
| 2 | Dar es salaam | Temeke | Dsm RVTSC | Ufundi Magari |
| | | | | Ufundi wa kutengeneza vifaa kutumia Aluminium |
| | | | | Ufundi Bomba |
| | | | | Umeme wa Majumbani |
| | | | | Uchomeleaji na Uungaji vyuma |
| | | | | Ukarabati wa bodi za magari |
| | | | | Ufundi Umeme wa Magari |
| | | | | Ushonaji |
| | | Kinondoni | Don bosco Oysterbay VTC | Ufundi magari |
| | | | | Useremala |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | | Uchorongaji vipuri |
| | | | | Ushonaji |
| 3 | Dodoma | Dodoma | Institute of Heavy Equipment and Technology (IHET) | Ufundi wa mitambo |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | | Umeme wa magari |
| | | | Don Bosco Dodoma Technical Institute | Useremala |
| | | | | Ufundi bomba |
| | | | | Uashi |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Uchorongaji vipuri |
| | | | | Ufundi umeme |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Umeme jua |
| 4 | Geita | Geita | Geita VTC | Umeme Majumbani |
| | | | | Ufundi Magari |
| | | | | Ufundi Bomba |
| | | | | Uashi |
| 5 | Iringa | Iringa | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ilula | Umeme wa majumbani |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | Mufindi | Mafinga Lutheran Vocational Training Centre | Ufundi magari na Mitambo |
| | | | | Uchomeleaji na Uungaji wa Vyuma |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ushonaji |
| | | Kilolo | RDO Kilolo VTC | Umeme wa Majumbani |
| | | | | Upishi |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Useremala |
| | | | | Uashi |
| 6 | Kagera | Biharamulo | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Rubondo | Umeme wa majumbani |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uashi |
| | | Misenyi | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera | Ufundi umeme |
| | | | | Uashi |
| | | | | Kilimo |
| 7 | Katavi | Mpanda | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya | Umeme wa Majumbani |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Kilimo |
| 8 | Kigoma | Kasulu | Kasulu DVTC | Ufundi umeme wa majumbani |
| | | | | Uashi |
| | | | | Ufundi Magari |
| | | | | Ushonaji |
| | | Kasulu | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kasulu | Ufundi umeme wa majumbani |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | | Umeme wa magari |
| | | | | Ufundi bomba |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi magari |
| | | Kakonko | Chuo cha Ufundi Stadi JKT Kasanda | Ufundi bomba |
| | | | | Ufundi umeme |
| | | | | Upishi |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi magari |
| | | Kigoma Vijijini | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kihinga | Umeme wa majumbani na viwandani |
| | | | | Uashi |
| | | | | Ushonaji |
| 9 | Kilimanjaro | Moshi Vijijini | Marangu School of Tourism and Vocational Training | Kuongoza watalii |
| | | | | Upishi |
| | | | | Huduma za kupokea wageni |
| | | | | Huduma za vyakula na vinywaji |
| | | Rombo | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mamtukuna | Uashi |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ufundi Magari |
| | | | | Umeme wa Majumbani |
| 10 | Lindi | Kilwa | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko | Umeme wa majumbani |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi Magari |
| | | | | Kuongoza Watalii |
| | | Ruangwa | Ruangwa DVTC | Ufundi umeme wa majumbani |
| | | | | Uashi |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi magari |
| 11 | Manyara | Mbulu | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tango | Umeme wa majumbani |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uashi |
| 12 | Mara | Musoma | St. Anthony Vocational Training Centre | Ushonaji |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | | Umeme wa magari |
| 13 | Mbeya | Mbeya Mjini | Chuo cha Ufundi Magereza Ruanda | Useremala |
| | | | | Uashi |
| | | | | Umeme wa majumbani |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| 14 | Morogoro | Morogoro | Lakewood Training Institute | Umeme wa majumbani |
| | | | | Kuongoza watalii |
| 15 | Mtwara | Masasi | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi | Umeme wa majumbani |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi bomba |
| | | | | Uashi |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| 16 | Mwanza | Ilemela | Mwanza RVTSC | Uchomeleaji na Uungaji vyuma |
| | | | | Ufundi Umeme wa Majumbani |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ufundi wa uchanganyaji na upakaji rangi |
| | | | | Ginnery Fitting |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Ufundi Bomba |
| | | Sengerema | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Sengerema | Ufundi Umeme |
| | | | | Uchomeleaji na Uungaji vyuma |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uashi |
| 17 | Njombe | Njombe | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Njombe | Umeme wa majumbani na viwandani |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi magari na mitambo |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | | Uashi |
| 18 | Pwani | Kibaha | Pwani RVTSC | Ufundi umeme wa majumbani |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ufundi umeme wa magari |
| | | | | Utengenezaji wa friji na Viyoyozi |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi magari |
| 19 | Rukwa | Sumbawanga | LAELA AGRICULTURE VTC | Kilimo cha mbogamboga (Horticulture) |
| | | | | Ufugaji (Animal Husbandry) |
| | | Sumbawanga | Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST - Rukwa) | Uchomeleaji na Uungaji vyuma |
| | | | | Uashi |
| | | | | Ufundi bomba |
| | | | | Ufundi Umeme wa Majumbani na Umeme Jua |
| 20 | Ruvuma | Mbinga | Chuo cha Ufundi Stadi Mpapa | Useremala |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Umeme |
| | | | | Uchomeleaji |
| | | Songea vijijini | Peramiho Vocational Training Center | Ushonaji |
| | | | | Ufundi Bomba |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ufundi Magari |
| | | | | Umeme wa Majumbani |
| 21 | Shinyanga | Kahama | Hill Forest College - Kahama | Front Office Operations |
| 22 | Simiyu | Bariadi | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bariadi | Umeme wa majumbani |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uashi |
| | | | | Useremala |
| 23 | Singida | Singida Mjini | Chuo cha Ufundi na Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu Sabasaba | Umeme wa Majumbani |
| | | | | Ushonaji Nguo |
| | | | | Ususi na Urembo |
| | | | | Uchomeleaji |
| | | | | Uokaji keki na mikate |
| | | Singida mjini | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida | Ufundi umeme |
| | | | | Ufugaji |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Ufundi magari |
| 24 | Tabora | Urambo | Urambo DVTC | Ushonaji |
| | | | | Uashi |
| | | | | Ufundi umeme wa majumbani |
| | | Nzega | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanhala | Umeme wa majumbani |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uashi |
| 25 | Tanga | Lushoto | St. Patrick's Vocational Training Centre | Ufundi Magari |
| | | | | Useremala |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Umeme wa magari |
| | | | | Umeme wa majumbani |
| | | Handeni | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Handeni | Ufundi umeme wa majumbani |
| | | | | Ufundi magari |
| | | | | Upishi |
| | | | | Ushonaji |
| | | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |

# JKT QUEENS YAPAA IVORY COAST IKITAKA FAINALI LIGI YA MABINGWA

**Na Shufaa Lyimo**

MSAFARA wa wachezaji 28 ukijumuisha viongozi wa Timu ya JKT Queens umeondoka leo alfajiri kuelekea nchini Ivory Coast kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa kwa wanawake yatakayoanza kutimua vumbi nchini humo kuanzia Jumapili wiki hii hadi Novemba 19, mwaka huu, huku ikipania kutinga fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Msemaji wa timu hiyo, Masau Bwire, alisema msafara huo utaondoka na wachezaji 21 pamoja na viongozi 7.

"Tunatarajia kuondoka kesho (leo alfajiri), kuelekea nchini Ivory Coast kwa ajili ya kwenda kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, ambayo yatashirikisha mabingwa wa Kanda za Soka Afrika," alisema Masau Bwire.

**Alisema kwa wale wachezaji wao 16 waliopo Timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars, wataondokea nchini Botswana leo kwenda moja kwa moja Ivory Coast kuungana na wenzao.**


Twiga Stars jana ilishuka dimbani nchini Botswana dhidi ya wenyeji wao hao, katika mchezo wa marudiano wa kuwania kufuzu michuano ya Olimpiki itakayofanyika mwakani nchini Ufaransa.

Bwire alisema maandalizi yao yamekamilika kuelekea kwenye mashindano hayo ambapo mchezo wao wa kwanza hatua ya makundi watacheza Jumapili dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini majira ya saa tano usiku.

"Mchezo wetu wa pili tutacheza Novemba 8, mwaka huu, dhidi ya Athletico FC, ambao ndio wenyeji wa mashindano hayo, na mchezo wa tatu tutakutana na Sporting Casablanca ya Morocco Novemba 11, mwaka huu," alisema msemaji huyo.

Aliongeza kuwa malengo yao ni kuingia fainali katika mashindano hayo ambayo yanashirikisha timu nane kutoka mabingwa kanda sita za mabingwa Afrika.






Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya 1245 Lounge and Restaurant, Sniper Mantana (kulia), akikabidhi kompyuta kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA'. **MPIGAPICHA WETU**

## JWTZ riadha waja na medali Majeshi Dunia

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Wanawake ya Riadha ya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) imeshika nafasi ya tatu kwenye mashindano Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM), yaliyomalizika Oktoba 29, mwaka huu, jijini Lucerne nchini Uswisi, huku ile ya wanaume ikimaliza katika nafasi ya 13.

Timu hiyo ikiwa na viongozi na wachezaji nane ilirejea nchini jana baada ya kushiriki mashindano hayo ya kimataifa.

Matokeo ya jumla ya timu kwa wanawake kati ya nchi (timu) 19, nchi ya Bahrain imetwaa medali ya dhahabu baada ya kuibuka mshindi wa kwanza, huku Morocco ikiondoka na medali ya fedha kwa kushika nafasi ya pili.

Kwa upande wa wanaume kati ya nchi (timu) 31, Morocco imetwaa medali ya dhahabu kwa kuibuka mshindi wa kwanza, huku Ufaransa ikiondoka na medali ya fedha baada ya kushika nafasi ya pili na ya tatu ikienda kwa Italia iliyozawadiwa medali ya shaba.

Matokeo mengine ya mchezaji mmoja mmoja kati ya wachezaji 91 kwa wanawake walioshiriki, Koplo Jepchumba Kilonzo (Bahrain) ndiye aliyeibuka mshindi wa kwanza na kubeba medali ya dhahabu, huku Sajenti Jebet Danies (Bahrain) naye akiondoka na medali ya fedha kwa kuibuka mshindi wa pili wakati Koplo Magdalena Shauri (Tanzania) arejea nchini na medali ya shaba, lakini Sajenti Taji Jackline Sakilu (Tanzania) naye akishika nafasi ya nne.

Kwa wanaume, kati ya wachezaji 123 walioshiriki, Sajenti El Aaraby Reda (Morocco) ndiye aliyebeba medali ya dhahabu kwa kushika nafasi ya kwanza huku Sajenti Alphonce Simbu (Tanzania) akishika nafasi ya pili na kuondoka na medali ya fedha wakati Sajenti Yassive El Alami (Morocco) akibeba medali ya shaba kwa kumaliza katika nafasi ya tatu.

Mbali na nchi hizo ambazo zimetwaa medali, zingine zilizoshiriki mashindano hayo ni pamoja na wenyeji Uswisi, Albania, Poland, Peru, Jamhuri ya Dominican, Brazil, Lithuania, Slovenia, Lativia, Chile, Ujerumani, Romania, Canada, Sweden, Uholanzi na Ubelgiji.

# *Mfuko Utamaduni, Sanaa na Michezo wapigwa jeki kompyuta*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kudhihirisha inatekeleza dhamira yake ya kusaidia maendeleo ya sekta ya utamaduni, sanaa na michezo nchini, Taasisi ya 1245 Lounge and Restaurant, maarufu kwa sifa yake ya kuandaa vyakula na burudani nzuri, imetoa msaada wa kompyuta mpakato kwenda kwa Mfuko wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia wizara hiyo. Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika katika ofisi za Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo jana ikiashiria hatua kubwa ya kuimarisha rasilimali za kidijitali kwa ajili ya michezo, utamaduni na shughuli za sanaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya 1245 Lounge and Restaurant, Sniper Mantana, akikabidhi kompyuta hizo kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa, na Michezo, Hamis Mwinjuma, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta za umma binafsi kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

"Tunafuraha kupata fursa ya kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan na juhudi za serikali za kukuza na kuendeleza sekta nzima ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

"Sekta za ubunifu na utamaduni ni sehemu muhimu ya jamii yetu, na tunaamini kwamba upatikanaji wa teknolojia ni muhimu sana katika ukuaji wake. Tunatumaini kuwa kompyuta hizi zitasaidia kuongeza uwezo wa wizara katika kuendeleza dhamira yake na kuleta matokeo mazuri katika maisha ya Watanzania. Kama 1245, tutaendelea kushirikiana na serikali katika kuijenga na kuiendeleza sekta hii sasa na siku za usoni," alisema Mantana.

Kwa upande wa Naibu Waziri, Mwana FA, alitoa shukrani zake kwa kusema: "Tunawashukuru Taasisi ya 1245 Lounge and Restaurant kwa mchango wenu mkubwa. Msaada huu wa kompyuta bila shaka utaimarisha juhudi zetu za kukuza utamaduni, sanaa na michezo ndani ya Tanzania.

Tunaamini zitaturahisishia kazi hasa katika kuungana na wasanii, taasisi za kitamaduni na vijana. Tunafurahi kuwa na washirika wa sekta binafsi kama vile 1245 Lounge and Restaurant ambao wanatuunga mkono katika dhamira yetu kwenye maendeleo ya sekta ya kitamaduni na kisanii".

## ZISIKUPITE

### REAL MADRID NA KEPA

REAL Madrid iko tayari kujadiliana na Chelsea kuhusu mkataba wa kudumu wa Kepa Arrizabalaga, 29, lakini hawatalipa zaidi ya euro milioni 17.5 kwa kipa huyo Mhispania ambaye aliwagharimu 'The Blues' takriban euro milioni 71.6 miaka mitano iliyopita. ***(Sun)***

### MSHAHARA WA POGBA

KLABU ya Juventus huenda ikatumia mshahara uliookolewa kwa kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba, 30, kumpata kiungo wa Arsenal Thomas Partey, 30, katika mkataba wa mkopo Januari. Pogba anakabiliwa na adhabu ya kufungiwa kwa muda mrefu kutojihusisha na soka ambayo itasababisha kupunguzwa kwa mshahara kutoka kwa Juve. ***(Mirror)***

### ARTETA ATAKA NYOTA

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, ameripotiwa kuwaongeza viungo Martin Zubimendi, 24 wa Real Sociedad na Hispania na Aurelien Tchouameni, 23 wa Real Madrid na Ufaransa kwenye orodha ya walengwa katika usajili wa Januari. ***(Calciomercato)***

### WIRTZ ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Florian Wirtz, kutoka Bayer Leverkusen huku Manchester City pia wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Express)***

### CHELSEA NA MAMADASHVILI

CHELSEA ilituma maskauti kumtazama mlinda mlango wa Georgia na Valencia, Giorgi Mamadashvili, 23, kwenye mechi ya timu hiyo ya Hispania dhidi ya Granada Jumapili. ***(90 min)***

### POCHETTINO AMTAKA SIMON

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino pia anavutiwa na kipa wa Athletic Bilbao na Hispania, Unai Simon, 26. ***(Fichajes)***

### OSIMHEN KUFUNGWA NAPOLI

NAPOLI iko tayari kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, 24, huku Liverpool wakihusishwa na mchezaji huyo. ***(Fichajes)***

### CHALOBAH AIITA DORTMUND

BEKI wa Chelsea na England, Trevor Chalobah, 24, amevutiwa na Borussia Dortmund. ***(Sun)***

### MUBAMA AIGOMEA WEST HAM

MSHAMBULIAJI wa England, Divin Mubama, 19, amekataa kuongezewa mkataba katika Klabu ya West Ham wakati akiwa amebakisha mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa. ***(The Athletic)***

### CATAMO AWANIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inamfuatilia winga wa Sporting Lisbon na Msumbiji, Geny Catamo, 22. ***(Birmingham Live)***

### DIAZ SOKONI KWA MIL. 20

ASTON Villa na West Ham wameambiwa na Real Madrid kwamba lazima walipe takriban euro milioni 20 kama wanataka kumsajili kiungo mshambuliaji mzaliwa wa Hispania, Brahim Diaz, 24. ***(Birmingham Mail).***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI: BALLON D'OR YA 8 NI MAALUM KWA MARADONA

## Pia awapongeza Haaland na Mbappe, akisema walistahili kushinda huku akiwatabiria...

**PARIS,** Ufaransa

BAADA ya Lionel Messi kushinda tuzo yake ya nane ya Ballon d'Or, amesema ni maalum kwa gwiji Diego Maradona na zaidi kwa wote waliofanikisha yeye kufikia hapo.

**Akizungumza mara baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo juzi usiku nchini Ufaransa, Messi alisema: "Leo (juzi) nilitaka kumtaja Diego. Hakuna mahali pazuri zaidi pa kumtakia heri ya kuzaliwa hapa karibu na watu wengi wanaopenda soka, kama alivyotaka. Popote ulipo, Diego... heri ya kuzaliwa. Hii inaenda kwako pia."**

"Familia yangu na marafiki, ningependa kuwashukuru kwa kila kitu ambacho mmefanya ili kutimiza ndoto zangu kwa miaka hii na kufikia ndoto ya Kombe la Dunia.

"Ballon d'Or zangu zote za 8 ni maalum, lakini la muhimu zaidi ni tuzo za pamoja.

"Sikuwahi kufikiria ningekuwa na kazi hii, nimebarikiwa na yote hayo na nadhani ni ngumu sana."

Pia Messi akazungumzia kuhusu kustaafu: "Kustaafu? Sijui kwa kweli. Nimekuwa nikizungumza sana hivi karibuni, lakini nataka kuendelea na kufurahia.

"Siwezi kuweka tarehe maalum kuna mabadiliko ya soka kila siku. Kama nilivyosema, mimi napenda soka na ninataka kuendelea."

Halafu akawazungumzia wapizani wake kwenye tuzo hiyo, Erling Haaland na Kylian Mbappe: "Haaland na Mbappe watashinda Ballon d'Or siku moja.

"Erling alistahili sana pia, ameshinda Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya huku akiwa mfungaji bora wa kila kitu. Tuzo hii ingeweza kuwa yako leo pia... Nina hakika katika miaka ijayo utashinda."

"Tuzo hii inakuja sambamba na kile ambacho kimefikiwa na timu ya Argentina. Hii ni zawadi kwa wachezaji, wafanyakazi na makocha na watu wote nchini Argentina.

"Nilikuwa na bahati kuwa kwenye timu bora zaidi duniani, katika klabu bora, timu bora zaidi katika historia Barcelona."

Messi ambaye ni mchezaji wa Inter Miami ya Marekani mwenye umri wa miaka 36, ameweka rekodi ambayo inaweza kuchukua miaka mingi kuvunjwa kwa kubeba mara nane.

Katika tuzo hizo, Kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England na Real Madrid, Jude Bellingham, alishinda mchezaji bora wa dunia mwenye umri wa chini ya miaka 21, huku Haaland akitwa tuzo ya mshambuliajin bora.

# UNITED WAHOFIA KUKOSA NNE BORA



**MANCHESTER,** England

MAOFISA wa Manchester United tayari wana wasiwasi kuhusu kumaliza katika nafasi nne za juu msimu huu, baada ya kufungwa na Manchester City, kwa mujibu wa ESPN.

Ushindi wa mabao 3-0 wa Man City katika Uwanja wa Old Trafford Jumapili, uliiacha United katika nafasi ya nane kwenye msimamo pointi 11 nyuma ya vinara Tottenham Hotspur na pointi nane nyuma ya nafasi za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Imezua hofu ndani ya klabu hiyo kwamba wanakabiliwa na msimu mwingine nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kushindwa kufuzu mara nne katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Kwa mujibu wa ESPN United bado wana imani kwamba kocha, Erik ten Hag, anaweza kubadilisha mambo, ingawa kuna kukubalika kwamba kiwango kitahitaji kuboreshwa sana ikiwa wanataka kumaliza katika nafasi nne za juu msimu huu.

United jana Jumatano ilikuwa ikicheza na Newcastle United kwenye Kombe la Carabao kabla ya mechi za ugenini dhidi ya Fulham na FC Copenhagen kwenye Ligi ya mabingwa.

Mchezo wao wa mwisho kabla ya mapumziko ya kimataifa ya Novemba ni dhidi ya Luton Town katika Uwanja wa Old Trafford.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba United wana matumaini ya kuwa na Aaron Wan-Bissaka kabla ya mapumziko baada ya kukosa mechi tisa zilizopita kutokana na jeraha la misuli ya paja huku Casemiro, ambaye alikosa mechi ya Manchester 'Dabi' kutokana na tatizo la kifundo cha mguu, pia anakaribia kurejea.

# Saka amjibu Arteta kucheza zaidi



**LONDO,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Bukayo Saka amesisitiza kuwa yuko tayari kujibu changamoto ya kocha Mikel Arteta ya kucheza mechi 70 msimu huu.

Winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 22, aliwaongoza 'Washikabunduki' hao katika ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Sheffield United Jumamosi na kuwaweka ndani ya pointi mbili nyuma ya vinara wa ligi, Tottenham Hotspur

Saka ameanza mechi zote isipokuwa moja ya Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Kuhusu kuichezea klabu hiyo mechi nyingi, Saka alisema: "Nadhani inawezekana. Ukiangalia wachezaji wa juu, wapo kila baada ya siku tatu na wanashinda michezo kwa timu yao.

"Kwa hiyo ninajaribu kuwa katika kiwango hicho na ni wazi kuwa katika kiwango hicho ninahitaji kujisukuma mwenyewe.

"Mimi ni mvulana ambaye siku zote nataka kuwa uwanjani, siku zote ninataka kujitolea kwa uwezo wangu wote, na ikiwa nitakuwa majeruhi na lazima nilazimishwe kuwa nje, basi bila shaka nitakaa nje.

"Lakini mradi nipo na niko tayari kucheza, siku zote nitajitolea kwa uwezo wangu wote na kuwaambia kuwa nataka kucheza."

Lakini kwa mara nyingine tena anaweza kuwa anavaa kitambaa cha unahodha wakati Arsenal itakaposafiri kwenda Newcastle kwenye Ligi Kuu Jumamosi.

Aliongeza: "Tunakaribia kilele cha jedwali la Ligi Kuu, tuko vinara wa Kundi letu la Ligi ya Mabingwa na bado tuko kwenye mashindano mengine yote.

"Nadhani hilo ni jambo ambalo tunaweza kujivunia, lakini nakubali kuna kiwango kingine cha sisi kwenda."

# Rais TFF ya Hispania afungiwa miaka mitatu

**NYON,** Uswisi

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka la Hispania, Luis Rubiales, amefungiwa kutojihusisha na soka kwa muda wa miaka mitatu kwa sababu ya kumpiga busu la mdomoni mchezaji wa kike baada ya fainali ya Kombe la Dunia la Wanawake 2023, FIFA imetangaza.

Kamati ya Nidhamu ya FIFA hapo awali ilikuwa imemsimamisha Rubiales kwa siku 90 baada ya kitendo chake - kumbusu fowadi Jenni Hermoso kwenye midomo, wakati Hispania ilipotwaa Kombe la Dunia kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya England mjini Sydney Agosti 20, mwaka huu.

Rubiales awali alikataa kuitikia wito wa kujiuzulu, lakini baada ya FIFA kumsimamisha kazi, Serikali ya Hispania ilijaribu kumtaka aondolewe kwenye wadhifa wake na Hermoso akawasilisha malalamiko yake na alijiuzulu Septemba 10, mwaka huu.

"Kamati ya Nidhamu ya FIFA imemfungia aliyekuwa rais wa Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), Luis Rubiales, kwa miaka mitatu kujihusisha na masuala ya soka katika ngazi ya kitaifa na kimataifa baada ya kubaini kuwa alikiuka kifungu cha 13 cha FIFA. Kanuni za Nidhamu," FIFA ilisema katika taarifa yake.

"Kesi hii inahusiana na matukio yaliyotokea wakati wa fainali ya Kombe la Dunia la Wanawake la FIFA mnamo Agosti 20, 2023, ambapo Rubiales alikuwa amesimamishwa kwa muda wa siku 90 awali.

"Rubiales amejulishwa kuhusu masharti ya uamuzi wa Kamati ya Nidhamu ya FIFA. Kwa mujibu wa vifungu husika vya Kanuni ya Nidhamu ya FIFA, ana siku kumi za kukata rufaa. FIFA inasisitiza dhamira yake kamili ya kuheshimu na kulinda uadilifu wa watu wote na kuhakikisha kuwa kanuni za msingi za maadili mema zinafuatwa."

Rubiales alisema atatumia haki yake ya kukata rufaa, akiituhumu FIFA kwa kutompa nafasi ya kujitetea.



HABARI MICHEZO

# YAO KINARA 'ASSIST' LIGI KUU, DIARRA 'CLEAN SHEETS', MIQUISSONE HATARI

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Yanga raia wa Mali, Djigui Diarra, anaongoza kwa kucheza mechi nyingi za Ligi Kuu Tanzania Bara bila nyavu zao kutikiswa (clean sheets), huku beki wa kulia wa timu hiyo, raia wa Ivory Coast, Yao Kouassi, akiongoza kwa kutoa pasi za mwisho zilizozaa mabao mpaka sasa.

Kiungo mshambuliaji wa Simba, Luis Miquissone pamoja na kutopata muda mwingi wa kucheza kwenye kikosi chao, mara kwa mara akiingia akitokea benchi huku baadhi ya mashabiki wakidai bado hayupo fiti, anashika nafasi ya pili kwa kutoa pasi za mwisho 'assist' akiwazidi wachezaji wengi wanaopata muda mrefu wa kucheza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Ligi zilizotolewa juzi, Diarra ana 'clean sheets' nne mpaka sasa ambazo alizipata katika mechi Yanga ilicheza dhidi ya JKT Tanzania na kushinda mabao 5-0, Geita Gold mabao 3-0, Namungo bao 1-0, na Singida Fountain Gate FC mabao 2-0.

**Kipa wa Azam, Idrissu Abdulai raia wa Ghana na John Noble, Mnigeria anayeidakiwa Tabora United, wanashika nafasi ya pili wakiwa na 'clean sheets' tatu kila mmoja.**

Makipa wenye 'clean sheets' mbili kila mmoja kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ni Mkongomani Ley Matampi wa Coastal Union, Erick Johora wa Geita Gold, Ismail Salehe wa JKT Tanzania, Lameck Kanyonga na Hasheem Mussa wote wa Mashujaa FC, Beno Kakolanya wa Singida Fountain Gate, Daniel Mgore wa Dodoma Jiji, Selemani Fikirini wa Ihefu na Wibol Maseke wa KMC.

Upande wa 'assist', Kouassi anaongoza kwa kutoa pasi nne za mabao, Miquissone wa Simba na Ladaki Chasambi wa Mtibwa Sugar wakiwa na 'assist' tatu kila mmoja.

Wachezaji ambao wametoa pasi mbili za mabao na wapo kwenye kundi lililo kwenye nafasi ya tatu, ni Cheik Sidibe wa Azam FC, Kibu Denis, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala' wa Simba, Maxi Nzengeli na Mudathir Yahaya wa Yanga, Awesu Awesu wa KMC, Impiri Mbombo wa Tabora United, David Bryson wa JKT Tanzania na Jacob Massawe wa Namungo FC.

## *Balozi wa Uingereza aongeza mzuka dabi Simba, Yanga*

INATOKA UKURASA 24

leo ya michezo kwa klabu hiyo ikiwamo timu kubwa, soka la vijana na wanawake lakini pia na manufaa ya nchi.

"Ninatarajia baada ya ujio wa hapa pia ataendelea kutembelea kwa wenzetu (Yanga) hii ni baada ya kuweka ushabiki pembeni na sasa tukiangalia mustakabali wa soka letu la Tanzania ambalo limepiga hatua," alisema Try Again.

Kwa upande wa wachezaji, Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, kwa niamba ya wachezaji wenzake alimshukuru balozi huyo kwa kuwatembelea na kutoa sapoti katika kutimiza majukumu yako ya kila siku.

Baada ya ziara hiyo aliitembelea Klabu ya Yanga na kufanya mazungumzo na uongozi wa klabu hiyo chini ya rais Injinia Hersi Saidi na makamu wake, Arafat Haji.

KARIBU SANA!...



Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, akisalimiana na Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, baada ya kuitembelea jana na kushuhudia mazoezi ya timu hiyo katika Uwanja wa Mo Simba Arena uliopo Bunju, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *RT yaziombea leseni kimataifa mbio mbili*

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKISHO la Riadha Tanzania (RT), limesema kwa sasa wametuma maombi ya usajili rasmi wa mbio za marathon za CRDB na NBC, ili zitambulike kimataifa na kuwavutia wanariadha wengi zaidi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Makamu rais wa Shirikisho hilo, William Kallaghe, alisema wametuma maombi kwa Shirikisho la Riadha la Dunia kuomba kusajiliwa kwa mbio hizo ili ziungane na mbio za Kilimanjaro Marathon kuwa na leseni ya kimataifa.

"Kama tutafanikiwa, mbio hizi zitakuwa zikijulikana kimataifa na zitaitwa za kimataifa, faida yake kubwa, kwanza zitatambulika lakini pia zitawavuta wanariadha wengi duniani kuja kushiriki," alisema Kallaghe.

Aidha, alisema kutambulika rasmi kimataifa kutazifanya mbio hizo kutumika kwa wanariadha kusaka viwango vya kushiriki mashindano makubwa zaidi yakiwamo ya dunia.

"Hapa nataka niwaeleweshe watu, si kila mbio ni marathon, watu siku hizi wanaandaa mbio za kilometa 10 wanaita marathon, mbio za marathon ni zile za kilometa 42, hizi ndio marathon na zile za nusu yake za kilometa 21 zile tunaziita nusu marathon," alisema Kallaghe.

Kallaghe alisema kwa taasisi au watu wanaotaka kuanzisha mbio zozote ni vizuri kuwasiliana na RT kwa ajili ya kufuata taratibu na mbio hizo kutambulika.

"Kuna taratibu zake, riadha ni mchezo kama ilivyo michezo mingine ina kanuni na sheria zake, hivyo kwa taasisi inayotaka kuanzisha mbio zake ni lazima wawasiliane na sisi," alisema Kallaghe.

Alisema wanataka kuona Tanzania inakuwa na mbio zake za marathon zitakazokuwa zikitambulika duniani ambazo zitasaidia kuitangaza nchi na kuleta wageni.

## Gamondi hataki presha

INATOKA UKURASA 24

wa Ngao ya Jamii, tunaendelea kujipanga na kuwapa wachezaji mbinu zitakazotusaidia kupata ushindi," alisema Gamondi.

Aidha, Kocha huyo raia wa Argentina, alisema anafurahishwa na namna wachezaji wake wanavyojituma mazoezini na haoni presha yoyote kwao.

"Naomba tu mashabiki wetu wanaendelee kutusapoti, naamini utakuwa mchezo mzuri, tutacheza katika ubora wetu na katika mipango yetu," alisema Gamondi.

Simba itakuwa mwenyeji wa Yanga kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumapili, Novemba 5 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa majira ya saa 11 jioni.

Kwa upande wa Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya, ametamba kuwa hawako tayari kuona wanapoteza kwa mara nyingine tena kwenye mechi hiyo ya watani wa jadi.

Tangu msimu uliopita Yanga imepoteza mara mbili, ikiwamo mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ngao ya Jamii uliyopigwa Uwanja wa Mkwakwani, Tanga na Simba walitwaa ubingwa huo kwa mikwaju ya penalti.

Akizungumza na Nipashe jana, Mudathir alisema baada ya mchezo wao na Singida Fountain Gate FC, Kocha Gamondi amefanyia kazi madhaifu yao na ubora wa Simba.

# Michezo

Jumatano Novemba 1, 2023

Nipashe




Saka amjibu Arteta kucheza zaidi UKURASA 22




Lionel Messi, mshindi wa tuzo yake ya nane ya Ballon d'Or 2023, baada ya kuwabwaga Erling Haaland na Kylian Mbappe juzi walioingia naye fainali mwaka huu. Picha ndogo pembeni ni miaka ambayo ametwaa tuzo hiyo. **PICHA: MTANDAO**

## Gamondi hataki presha kwa wachezaji

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

ZIKIWA zimebaki siku nne tu kabla ya mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hana shaka na wachezaji wake katika kutimiza majukumu yao kwenye mchezo huo na hataki kuwapa presha.

Akizungumza jana, Gamondi, alisema anafahamu mchezo dhidi ya Simba ni tofauti na michezo mingine, lakini hataki kuwabebesha mzigo wa presha wachezaji wake badala yake anaendelea kuwapa mbinu zitakazowasaidia kufanya vizuri.

Alisema ameifuatilia Simba katika michezo mingi, hivyo anafahamu nini cha kuwapa wachezaji wake katika kukabiliana nao siku hiyo ya mchezo.

"Presha itoke kwa mashabiki labda, lakini mimi nauchukulia mchezo huu kama michezo mingine ingawa ni kweli ni mechi kubwa sana katika Ligi ya Tanzania, nataka wachezaji wangu wafanye kila wanachokifanya kila wakati kwenye michezo mingine, hii itasaidia kupunguza presha kwa wachezaji na kuwapa nafasi ya kutimiza majukumu yao," alisema Gamondi.

"Tunataka kushinda Jumapili hilo ndilo jambo la msingi, tulipoteza kwa penalti kwenye mchezo wetu

INAENDELEA UKURASA 23

# Balozi wa Uingereza aongeza mzuka dabi Simba, Yanga SC

### ●●● Azitembelea na kutinga mazoezini Bunju, aahidi makubwa na kwenda kuzishuhudia Jumapili...

**Na Saada Akida**

HUKU joto la 'Dabi' ya Kariakoo, likizidi kupanda Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, amezitembelea Klabu za Simba na Yanga katika ofisi zao Dar es Salaam na kisha kwenda kushuhudia mazoezi ya 'Wekundu wa Msimbazi' na kuzungumza na wachezaji katika Uwanja wa Mo Simba Arena, uliopo Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Simba na Yanga zinajiandaa na mchezo wa Dabi ya Kariakoo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili wiki hii, na ujio wa balozi huyu ambaye ameeleza wazi ni mpenzi mkubwa wa klabu ya Simba, ulipokelewa vizuri na wachezaji pamoja na viongozi wa timu hiyo.

**Balozi huyo aliyeambatana na viongozi wa Simba, wakiwamo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Salim Abdallah 'Try Again' na Ofisa Mtendaji Mkuu (CEO), Imani Kajula, kutembelea mazoezi ya timu hiyo, alisema kwa muda mrefu amekuwa akivutiwa na kuifuatilia klabu hiyo.**

Concar alisema Klabu ya Simba ni moja ya klabu zinamvutia nchini na anaiona ikizidi kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa na kwamba amefurahi kutembelea klabu hiyo, kikubwa ni kuzungumzia maendeleo ya mpira wa miguu kwa ngazi ya klabu na taifa kwa jumla.

Alisema anapenda sana soka, amekuwa akifuatilia klabu hiyo kuanzia ngazi ya soka la vijana na wanawake kwa kufanya vizuri na kuitembelea ni kuweza kujadili maendeleo ya soka ikiwamo kukuza soka la vijana.

"Nimefurahi kutembelea Simba, nimfuatiliaji mzuri wa soka ndio maana nimekuja hapa kubadilisha uzoefu na viongozi wa klabu hii.

"Ujio wangu ndani ya klabu hii utasaidia katika programu za soka la vijana na wanawake, lakini pamoja na kuona klabu hii inazidi kuwa kubwa na kufanya makubwa," alisema Concar.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Try Again, alisema ushiriki wa klabu hiyo na kuonyesha kiwango kizuri katika michuano ya kimaitafa ikiwamo Afrika Football League (AFL), imemvutia balozi huyo kuitembelea.

Alisema ushiriki wa AFL umefungua milango kwa klabu hiyo kupata ugeni wa balozi huyo na kujadiliana mambo mbalimbali ya maendeleo ya michezo hapa nchini ikiwamo soka la wanawake na vijana.

"Ujio wa Balozi David Concar utaleta neema kwa Simba baada ya kujadiliana maende-

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >